# Nipashe

Ijumaa Novemba 24, 2023 • Tanzania 1000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581504

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


BUFE
IJUMAA NOVEMBA 24, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Usakaji pesa unavyowaondoa kinamama Njombe kwenye jukumu kuu kunyonyesha vichanga vyao

**Mapinduzi kilimo kahawa, Rais alipotanua soko China, nyumbani ofa miche 600,000**

Akubaliana na Rais Mwenza wauzaji kujisajili Kigoma, Katavi wachangamkia fursa uzalishaji

UKURASA 11

**WAHITIMU** wa SUA wamlilia mwenzao aliyefia vitani Israel

UKURASA 3

**MBARAWA** ashtuka timuatimua TASAC



UKURASA 7

**TB** bado tishio kwa afya nchini, takwimu zashtua

UKURASA 18


## MATOKEO LA VII

# Kiingereza, Hisabati bado hali ni mbaya

UKURASA 2



Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Ally Mohamed, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitangaza matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi (PSLE) 2023. **PICHA: JOHN BADI**




Idadi ya watahiniwa waliopata alama D kwa miaka miwili. **JEDWALI NA SALOME KITOMARI**

# Mpoki kufungua kesi nane kumshtaki Jaji

**KUHUSU** kusimamishwa uwakili, wanasheria 25 kumsaidia ... *Endelea Uk. 2*



## Apendekeza wanaonajisi na kulawiti wahasiwe

UKURASA 17

**MICHEZO** **GRIEZMANN HANA MPANGO KUONDOKA ATLETICO** UK. 22

**KATUNI** UK. 6

# Kiingereza, Hisabati hali mbaya

**Na Romana Mallya**

MASOMO ya Kiingereza na Hisabati bado ni tatizo kubwa kwa wanafunzi wengi nchini. Hili linadhihirishwa na matokeo ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) mwaka huu yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

Kwa mujibu wa matokeo hayo yaliyotangazwa katika ofisi za NECTA mkoani Dar es Salaam jana na Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Dk. Said Mohamed, kati ya watahiniwa 1,356,207 waliofanya mtihani huo Septemba mwaka huu, asilimia 61.44 wameambulia daraja D (wamepata alama 11-20) katika somo la Kiingereza.

Hali hiyo pia imeshuhudiwa katika somo la Hisabati ambalo kati ya watahiniwa 1,356,216, asilimia asilimia 51.02 wamepata daraja D katika somo hilo, ikiwa ni zaidi ya nusu ya watahiniwa hao.

Masomo hayo yameonekana kuwa tatizo kwa wanafunzi wengi kwa kuwa hata mwaka jana (2022) ufahulu katika masomo hayo ulikuwa wa kusuasua.

Kwa mwaka jana, asilimia 67.71 ya watahiniwa 1.347,933 walipata daraja D katika somo la Kiingereza huku asilimia 45.51 ya watahiniwa 1,347,982 wakipata alama za daraja D katika somo la Hisabati.

Katika matokeo ya mwaka jana Kiingereza waliopata daraja E ni asilimia 2.9 wakati mwaka huu asilimia 4.21 ya watahiniwa wamepata alama za daraja hilo (0-10).

Kwa somo la Hisabati, asilimia 1.21 walipata alama za daraja E na mwaka huu, asilimia 0.15 wamepata daraja E katika somo hilo.

Somo lingine ambalo ni tatizo ni Sayansi na Teknolojia ambalo kati ya watahiniwa 1,356,230, wa mwaka huu, asilimia 23.01 wamepata alama D huku mwaka 2022 asilimia 26.71 ya watahiniwa 1,347,993 walipata alama za daraja hilo.

Ufaulu hauridhishi pia katika somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi ambalo kwa mwaka huu waliopata D ni asilimia 21.82 ya watahiniwa 1,356,224 huku mwaka 2022 asilimia 26.25 ya watahiniwa 1,347,973 walipata alama za daraja hilo.

Masomo ambayo wanafunzi wamefanya vizuri ni Kiswahili; waliopata daraja D ni asilimia 9.15 ya watahiniwa 1,356,140, huku mwaka 2022 asilimia 7.74 ya watahiniwa 1,347,979 walipata alama za daraja hilo.

Somo la Uraia na Maadili mwaka huu asilimia 14.05 ya watahiniwa 1,356,228 wamepata alama D, wakati mwaka 2022 asilimia 15.04 ya watahiniwa 1,347,991 walipata alama hizo.

**WADAU WAFUNGUKA**

Meneja wa Idara ya Utafiti na Uchambuzi wa Sera wa Shirika la HakiElimu, Mwemezi Makumba, akizungumza na mwandishi baada ya kutangazwa matokeo hayo, alisema watahiniwa kufanya vibaya kunatokana na kutokuwapo walimu wa kutosha na wenye weledi katika masomo ya Kiingereza na Hisabati.

Alitaja tatizo lingine ni mbinu za ufundishaji, akisisitiza uwekezaji unahitajika katika mazingira ya kujifunzia.

> **Somo lingine ambalo ni tatizo ni Sayansi na Teknolojia ambalo kati ya watahiniwa 1,356,230, wa mwaka huu, asilimia 23.01 wamepata alama D huku mwaka 2022 asilimia 26.71 ya watahiniwa 1,347,993 walipata alama za daraja hilo.**

"Changamoto nyingine ni msongamano mkubwa wa wanafunzi darasani katika shule za serikali unaosababisha kuwapo ufuatiliaji mdogo kwa watoto na kuchangia wanafunzi kutoiva katika masomo.

"Maeneo haya yote yanahitajika kufanyiwa kazi ili kutibu tatizo hili. Tusipowekeza, hata matokeo ya mwakani yatakuwa hivi," alitahadharisha.

**WAFUTIWA MATOKEO**

Katika hatua nyingine, NECTA imefungia vituo viwili vya mtihani ambavyo ni Twibhoki (PS0904095) na Graiyaki (PS0904122), vyote vya Halmashauri ya Serengeti mkoani Mara, vilivyothibitika kupanga kufanya udanganyifu katika mtihani.

Katibu Mtendaji Dk. Mohamed alisema baraza limefuta matokeo yote ya watahiniwa 31 sawa na asilimia 0.002 ya watahiniwa 1,356,392 waliofanya mtihani huo mwaka huu kutokana na kufanya udanganyifu.

Pia alisema baraza limeviandikia barua za onyo vituo vya mtihani vinne ambavyo ni Mother of Mercy (PS0203133), St. Mary's Mbezi Beach (PS0203088) vya Halmashauri ya Kinondoni, Dar es Salaam; Charm Modern (PS0103111) cha Halmashauri ya Karatu, Mkoa wa Arusha; na Morotonga (PS0904042) cha Halmashauri ya Serengeti, Mkoa wa Mara.

Alisema vituo hivyo vilijaribu kujihusisha na vitendo vya udanganyifu katika mtihani huo, hivyo vitakuwa chini ya uangalizi wa baraza mpaka litakapojiridhisha kuwa ni vituo salama vya uendeshaji Mtihani wa Taifa.

"Baraza limezuia kutoa matokeo ya watahiniwa 360 ambao walipata matatizo ya afya na kushindwa kufanya mtihani kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo. Wamepewa fursa kufanya mtihani mwaka 2024," alisema.

Dk. Mohamed alisema jumla ya watahiniwa 1,397,293 walisajiliwa kufanya mtihani huo, wakiwamo wasichana 742,690 sawa na asilimia 53.15 na wavulana 654,603 sawa na asilimia 48.85.

Alisema kati ya watahiniwa waliosajiliwa, wenye mahitaji maalum ni 4,599 sawa na asilimia 0.33.

"Kati ya watahiniwa 1,397,293 waliosajiliwa, watahiniwa 1,356,392 sawa na asilimia 97.07 walifanya mtihani wakiwamo wasichana 726,078 sawa na asilimia 97.76 na wavulana ni 630,630 sawa na asilimia 96.29," alisema.

Alisema watahiniwa 40,901 sawa na asilimia 2.93 hawakufanya mtihani, kati yao wavulana ni 24,289 sawa na asilimia 3.71 na wavulana ni 16,612 sawa na asilimia 2.24.

**UFAULU WA JUMLA**

Dk. Mohamed alisema jumla ya watahiniwa 1,092,960 sawa na asilimia 80.58 ya watahiniwa waliofanya, wamefaulu kwa kupata daraja A, B na C ambapo kati yao, wavulana ni 507,920 sawa na asilimia 80.59 na wasichana ni 585,040 sawa na asilimia 80.58.

Alisema mwaka 2022 watahiniwa waliofaulu walikuwa ni 1,073,402 sawa na asilimia 79.62. hivyo, ufaulu wa jumla umeongezeka kwa asilimia 0.96.

"Katika ubora wa ufaulu, watahiniwa wengi wamepata daraja B na C. Daraja B ni watahinwa 314,646 sawa na asilimia 23.2, daraja C ni watahiniwa 724,371 sawa na asilimia 53.41 na watahiniwa 53,943 sawa na asilimia 3.98 wamepata daraja A," alisema.

Alisema ubora wa ufaulu kwa wasichana umeongezeka kwa kiasi kikubwa hadi asilimia 80.58 kulinganishwa na asilimia 78.91 katika mwaka 2022 ambapo ongezeko katika daraja A ni asilimia 0.13, daraja B ni asilimia 0.96 na daraja C ni asilimia 0.57

Kwa upande wa wavulana, Katibu Mtendaji alisema ubora wa ufaulu umeongezeka hadi asilimia 80.59 kulinganishwa na asilimia 80.41 katika mwaka 2022 ambapo ongezeko katika daraja A ni asilimia 0.42 na daraja B ni asilimia 0.58.

"Ufaulu wa daraja C umeshuka kwa asilimia 0.83. Kwa ujumla ufaulu wa wavulana na wasichana umefanana, wavulana wamefaulu kwa asilimia 80.59 na wasichana kwa asilimia 80.58," alifafanua.

**UFAULU KIMASOMO**

Dk. Mohamed alisema ufaulu wa somo la Kiingereza ni asilimia 34.35 na ufaulu wa somo la Kiswahili ni asilimia 87.91, akifafanua kuwa kwa somo la Kiingereza umepanda kwa asilimia 4.96 na Kiswahili umeshuka kwa asilimia 1.59 kulinganishwa na mwaka 2022.

"Katika somo la Kiingereza wavulana wanaufaulu wa asilimia 34.39 na wasichana wana ufaulu wa asilimia 34.32 na somo la Kiswahili wasichana wana ufaulu mkubwa wa asilimia 88.91 kuliko wavulana ambao wana ufaulu wa asilimia 86.76.

"Ubora wa ufaulu, somo la Kiswahili umeongezeka kwa watahiniwa walipata daraja A hadi asilimia 30.44 kulinganishwa na asilimia 29.96 mwaka 2022 japokuwa idadi ya watahiniwa waliopata daraja B imepungua kwa asilimia 2.01," alisema.

Alisema katika somo la Kiingereza, ubora wa ufaulu umeongezeka kwa watahiniwa waliopata daraja A na B hadi asilimia 11.4 kulinganishwa na asilimia 8.65 mwaka 2022.

**SAYANSI, HISABATI**

Katibu Mtendaji alisema ufaulu wa somo la Sayansi na Teknolojia ni asilimia 74.08 na la Hisabati ni asilimia 48.83, hivyo umepanda kwa asilimia 2.45 katika somo la Sayansi na Teknolojia na kwa Hisabati umeshuka kwa asilimia 4.46 kulinganishwa na mwaka 2022.

Alisema somo la Sayansi na Teknolojia, wavulana wana ufaulu wa asilimia 75.78 na wasichana wana ufaulu wa asilimia 72.6 na somo la Hisabati wavulana wana ufaulu mkubwa wa asilimia 52.45 kuzidi wasichana wenye asilimia 45.69.

Alisema ubora wa ufaulu somo la Sayansi na Teknolojia umeongezeka kwa watahiniwa waliopata daraja A na B hadi asilimia 28.11 kulinganishwa na asilimia 26.32 mwaka 2022.

Alisema katika somo la Hisabati, ubora wa ufaulu umeshuka kwa watahiniwa waliopata daraja A na B hadi asilimia 10.88 kulinganishwa na asilimia 13.1 mwaka 2022.

"Pamoja na ubora wa ufaulu wa somo la Hisabati kushuka, ufaulu wa watahiniwa walipata daraja A umeongezeka kwa asilimia 0.33.

"Idadi ya watahiniwa waliopata daraja la mwisho ambalo ni E sawa na asilimia 0 hadi 10, imepungua kwa kiasi kikubwa hadi asilimia 0.15 kulinganishwa na asilimia 1.21 mwaka 2022," alisema.

Alisema idadi ya shule katika makundi ya umahiri inaonesha kuwa kati ya shule 18,314 zenye matokeo ya PSLE 2023, shule 13,833 sawa na asilimia 75.47 zimepata wastani wa daraja la C kulinganishwa na madaraja mengine ya ufaulu.

"Shule zilizopata wastani wa daraja A-C zimeongezeka kwa asilimia 1.71 kutoka shule 16,294 sawa na asilimia 91.02 mwaka 2022 hadi kufikia shule 16,984 sawa na asilimia 92.73 mwaka 2023. Hakuna shule zenye wastani wa daraja E," alisema.

Katibu Mtendaji alisema baraza limewasilisha matokeo hayo kwenye mamlaka zinazohusika ili zifanye uchaguzi wa watahiniwa wa kujiunga na elimu ya sekondari, hivyo matokeo yatatangazwa na mamlaka baada ya kukamilisha uchaguzi.


MKOMBOZI COMMERCIAL BANK

MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

TAARIFA KWA UMMA

KUHAMA KWA TAWI LA MT. YOSEFU

Tunapenda kuwataarifu wateja na wadau wetu wa thamani kuwa, tawi letu la Mt.Yosefu litahamia katika jengo jipya liitwalo St. Joseph House, gorofa ya chini iliyoko Plot No 40, Mtaa wa Mansfiled, nyuma ya Kanisa Kuu la Mt. Yoseph mnamo tarehe 27 Novemba 2023.

Tafadhali kumbuka kuwa anuani na namba za simu hazijabadilika

**Tawi la Mt. Yosefu,**
**Plot Na 40, Mtaa wa Mansfiled,**
**Nyuma ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Yosefu,**
**S.L.P 38448,**
**Dar es Salaam.**
**Simu: +255 22 2137806/7**

Tunaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaosababishwa na mabadiliko haya.

**Imetolewa na Menejimenti.**

## HABARI KITAIFA



Askari polisi wa kikosi cha usalama barabarani, Sajini Ninga Gilagiza, akimpima kilevi dereva wa basi la mikoani, kabla ya kuondoka katika Stendi Kuu ya Mabasi ya Nyegezi, jijini Mwanza jana alfajiri.
**PICHA: VITUS AUDAX**

# Wahitimu SUA wamlilia mwenzao aliyefia Israel

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAHITIMU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), wamesikitishwa na kifo cha aliyekuwa mhitimu mwenzao, Clemence Mtenga (22), aliyeuawa baada ya kutekwa na kikundi cha kigaidi cha Hamas nchini Israel kwenye shambulio la Oktoba 7, mwaka huu.

Mmoja wa wanafunzi wa kilimo biashara, kozi aliyokuwa akisoma Mtenga, Milanzi Shandries, alisema wakiwa na furaha kuhitimu salama huku wakiwa na huzuni kwa sababu mwenzao ameshindwa kutimiza ndoto zake baada ya kufariki dunia licha ya kuwa alikuwa mwenye kujituma na mpenda dini.

Alisema vijana wengi huwa wana ndoto na wanapohitimu, hutaka kuzitimiza lakini mwenzao ameondoka bila kutimiza ndoto zake.

Mhitimu mwenzake, Neema Magesa, alisema wanamshukuru Mungu kwa yote kwa kuwa wanahitimu na kwa bahati mbaya hawako na mwenzao kwenye kumaliza elimu yao.

Magesa alisema kifo cha mwenzao kimewaumiza na kusababisha kukosa furaha endelevu, hivyo kujigawa wengine kwenda msibani mkoani Kilimanjaro kwa ajili ya kuhani na wengine kubaki chuoni kwenye mahafali.

Alisema Mtenga alikuwa mtu mwenye kusaidia wenzie kwenye taaluma, mtu wa kushirikiana na wenzake na kwamba walikuwa pamoja katika kuandika utafiti mbalimbali chuoni hapo.

Mtenga na mwenzake mmoja ambaye bado hajarejea nchini na wala hajulikani aliko hadi sasa, alikwenda Israel Septemba, mwaka huu, kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo katika kilimo biashara kuelekea kukamilisha mitihani yake ya kumaliza mwaka wake wa tatu wa masomo chuoni hapo.

Makamu wa Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alisema wanachuo 3,095 wamehitimu shahada mbalimbali chuoni hapo na kuhudhurishwa na Mkuu wa Chuo hicho, Waziri Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba.

# Mpoki kufungua kesi nane kumshtaki Jaji

**Na Halfani Chusi**

ALIYEKUWA Wakili wa Boniface Mwabukusi, Mpale Mpoki, ametangaza kusudio la kufungua kesi nane dhidi ya Jaji Ntemi Kilekamajengo, kutokana na kusimamishwa kufanya kazi kwa miezi sita.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mpoki alisema anakusudia kufanya hivyo kwa kuwa jaji huyo katika kufikia uamuzi wa kumfungia, alioutoa Novemba 20, mwaka huu, hakuzingatia sheria na Katiba ya nchi.

Mpoki alisema kabla ya uamuzi huo, hakupewa nafasi ya kujitetea jambo ambalo lilimnyima haki za msingi, hivyo anakata rufani katika Mahakama Kuu ya Tanzania. Kutokana na kusudio hilo, alisema mpaka jana mawakili 25 walikuwa wamejitokeza kumtetea.

Baada ya kufungiwa, alisema mawakili wengine saba waliokuwa wakimtetea Mwabukusi katika shauri la kimaadili, pia walijitoa kwa kuhofiwa kukutwa na masahibu kama hayo. Hatua hiyo ilisababisha Mwabukusi kujitetea binafsi.

"Tayari tumeshapeleka mbele ya kamati barua ya kusudio la kukata rufani Mahakama Kuu na tumeandika barua kuomba nakala ya uamuzi huo kwa vile mwenendo na uamuzi uliotolewa siku hiyo hauzidi karatasi tatu za maandishi ya mkono. Ni matumaini yetu tutapata mwenendo huo ndani ya muda mfupi," alisema.

Endapo apo hukumu hiyo haitapatikana ndani ya siku 10 tangu siku ya barua hiyo, watawajibika kuomba amri ya kumlazimisha mwenyekiti awapatie nakala hizo mapema iwezekanavyo.

Licha ya kumshtaki mahakamani, alisema anatarajia haraka iwezekanavyo kuyafikisha malalamiko yake mbele ya Tume ya Maadili ya Utendaji wa Majaji, iliyoundwa chini ya Sheria Namba 4 ya mwaka 2011 na malalamiko hayo yataambatana na haki ya viapo vya mawakili wenzake aliokuwa nao siku ya tukio.

Pia alisema anakusudia kufungua kesi ya kikatiba Mahakama Kuu ya Tanzania, dhidi jaji huyo ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Taifa ya Maadili ya Mawakili, kwamba kumsimamisha amempokonya haki yake ya kufanya kazi.

Alilitaja kusudio lingine kuwa ni kufungua kesi nyingine ya kikatiba kupinga baadhi ya vifungu kadhaa vilivyomo ndani ya Sheria ya Mawakili vinavyopingana na haki ya asili ya kusikilizwa na kukinzana na ibara kadhaa za Katiba ya Tanzania.

"Nakusudia pia kufungua shauri katika Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki kwa kuwa kitendo cha kusimamishwa uwakili hakiendani na misingi ya Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama inavyoamrishwa kwenye Ibara 6(d) kuhusiana na nchi husika kukuza na kulinda haki za watu kama ilivyoainishwa katika tamko la Afrika la Haki za Binadamu," alisema.

Kusudio la sita, alisema anataka kuwashawishi wanachama wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kuitisha mkutano mkuu maalum wa chama ili kujadili mwenendo wa uonevu uliofanywa dhidi yake na uamuzi wa jaji na mawakili wengine waliopita mbele ya kamati hiyo kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita.

Mpoki pia alisema anakusudia kuandika barua kwa Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Mataifa, Margaret Salterthwale, juu ya kuporomoka kwa hali ya juu ya uhuru wa mawakili Tanzania hasa kutokana na uwapo wa sheria mbaya na kandamizi dhidi ya mawakili inayoondoa uhuru wa Mahakama Kuu unaoathiri utawala bora.

"Kusudio langu lingine, nitatoa taarifa kwa Mwangalizi Maalum wa Umoja wa Afrika (AU) juu ya utetezi wa haki kwa Mtaalamu Maalum wa Watetezi wa Haki za Kibinadamu Barani Afrika, Remmy Lumbu, kuangalia juu ya haki ya kazi za watetezi wa haki za binadamu na kuangalia ni jinsi gani haki za watetezi hao na maslahi ya kazi yatalindwa, ikiwezekana nipeleke malalamiko yangu kwenye Kamisheni ya Afrika ya Haki za Binadamu.

Sambamba na hayo, alisema anakusudia kumfungulia jaji huyo kesi ya fidia kwa muda atakaokaa bila kazi, hakutaja kiasi alichopanga kulipwa lakini alibainisha kuwa itategemeana na ushauri kutoka kwa mawakili wake.

**MZIZI WA TATIZO**

Akisimulia namna ilivyokuwa, Mpoki alisema walipoomba kukata rufani dhidi ya kesi ya mteja wake, Mwabukusi, ambaye alikuwa anashtakiwa kwa kuongea maneno yaliyokiuka maadili katika utendaji wa kazi, baada ya kesi yake kuhusu suala la bandari, jaji alipandisha ghadhabu na kumwuliza ni kwa nini anataka kukata rufani kwenye shauri ambalo sheria hairuhusu.

Nilimjibu kuwa rufani inaruhusiwa chini ya sheria na hayo ni maelekezo ya mteja wetu, nisingeweza kukataa kutoa kusudio la mteja wangu la kukata rufani. Jaji alijibu nimwelekeze kwa nini nakata rufani, nikamwambia kwa kuwa tumeshakaa muda mrefu mahakamani, tuahirishe kesi mpaka kesho nitakuja kukueleza.

"Basi mwenyekiti alisema kitendo changu cha kukubali kutoa kusudio la kukata rufani ni ukiukwaji wa maadili, hivyo ameamua kunichukulia hatua za kinidhamu pasipo kushirikisha wajumbe wengine wa kamati.

Aliinama kuandika na baada ya kuinuka akasoma kinachoitwa adhabu na kunihukumu kunifungia leseni yangu ya uwakili kwa miezi sita toka Novemba 20, 2023," alisema.

Mpoki aliishukuru TLS kwa kupinga hatua iliyochukuliwa dhidi yake, akisisitiza bado inaendela kumsaidia kwa nguvu zote ikiamini kuwa kitendo hicho ni shambulizi dhidi yake bali ni dhidi ya mawakili wote Watanzania na dhidi ya uhuru wa wanasheria.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA MAJARIBIO (PILOT) WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA 'BIOMETRIC VOTER'S REGISTRATION (BVR) KUANZIA TAREHE 24/11/2023 HADI 30/11/2023 KATIKA KATA ZA IKOMA NA NG'AMBO**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote wa kata ya Ikoma iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, Mkoani Mara na Kata ya Ng'ambo iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Mkoa wa Tabora kuwa, Uboreshaji wa Majaribio (PILOT) wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura utafanyika kwa siku saba kwa kila kituo.

1. **SIKU:** Wananchi watajiandikisha na kurobresha taarifa zao kuanzia siku ya Ijumaa tarehe 24 hadi Alhamisi 30 Novemba, 2023
2. **VITUO:** Uandikishaji wapiga kura utafanyika katika vituo vitakavyoainishwa na Tume.
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa kuanzia saa 2:00 kamili Asubuhi na kufungwa saa 12:00 kamili Jioni

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGAKURA UTAHUSISHA MAMBO YAFUATAYO; -**

1. Kuandikisha wapiga kura wapya waliotimiza umri wa Miaka 18 ambao ni raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria.
2. Kuandikisha wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 ifikapo uchaguzi Mkuu 2025.
3. Kuandikisha wale ambao wanazo sifa lakini hawakujiandikisha hapo awali.
4. Kuboresha taarifa za Wapiga kura waliohama Kata au Majimbo yao ya Uchaguzi au ambao taarifa zao zilikosewa hapo awali Mf. Majina
5. Kwa wale wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa binafsi na wanaohama vituo au vyote viwili kwa wakati mmoja wanaweza pia kuanzisha mchakato wa kuboresha taarifa zao kwa kwa njia ya mfumo wa mtandao 'online'. Mfumo huu wa kuboresha taarifa za mpiga kura unapatikana katika mtandao wa Tume - www.nec.go.tz kwa kutumia kompyuta au simu janja kisha atabonyeza kiunganishi (link) iliyoandikwa "Boresha Taarifa za Mpiga Kura" au atatumia anuani ya ovrs.nec.go.tz itakayompeleka moja kwa moja kuanzisha mchakato huo. Katika mfumo huu, wapiga kura wanatakiwa kuingiza namba ya kitambulisho cha taifa (NIN), namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu anayotumia kwa sasa na jina la kata kisha watapata ujumbe wenye namba ya utambulisho (token namber) ambayo wataenda nayo kituoni ili kukamilisha taratibu za kupata kadi ya mpiga kura.
6. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura waliopoteza kadi zao au kuharibika.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kujiandikisha au kuboresha taarifa zao itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokuwa nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituoni atachukuliwa alama ya vidole vyote kumi vya mikono yote miwili na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Kwa Mpiga Kura aliyeboresha taarifa zake mtandaoni ni muhimu akahifadhi vyema namba ya kumbukumbu (token) ili iweze kumsaidia kupata kadi yake anapokwenda katika kituo cha kujiandikisha.

Tumia haki yako ya msingi kwa kwenda kujiandikisha.

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

217722802




Mkurugenzi wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku akizungumza wakati wa maadhimisho ya miaka 75 ya Tamko la Azimio la Haki za Binadamu, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam jana, yenye kauli mbiu ya "Kutafakari upya siku za nyuma, mustakabali wa ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Serikali yaokoa milioni 60/- kwa kila mgonjwa wa figo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI sasa inaokoa Sh. milioni 60 kwa kila mgonjwa wa figo aliyekuwa anapelekwa kupandikizwa figo nje ya nchi kutokana na kuimarishwa huduma hizo nchini.

Vilevile, imesema matibabu ya figo tangu yaanzishwe nchini, wagonjwa zaidi ya 100 wamepandikizwa figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Katika ufunguzi wa kongamano la Tisa la Madaktari Bingwa wa Figo, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Prof. Pachal Ruggajo alisema jana kuwa serikali imepunguza gharama kubwa iliyokuwa inatumika kupeleka wagonjwa wa figo nje ya nchi baada ya kuwekeza katika sekta ya afya nchini.

"Tunashukuru sana serikali kwa uwekezaji inaofanya katika sekta ya afya, tunawashukuru pia madaktari na wauguzi kwa kazi nzuri ya kuwahudumia wagonjwa wa figo," alisema Prof. Ruggajo.

Alibainisha kuwa hivi sasa wagonjwa wa figo wanapatiwa matibabu nchini kwa gharama nafuu hadi mgonjwa anapopona na kurejeshwa nyumbani.

Akizungumzia utoaji tiba kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo, mkurugenzi huyo alisema inatolewa BMH na Muhimbili, hivyo Watanzania wanatakiwa kwenda kufanya uchunguzi ili kubaini kama wako salama na kuongeza kuwa madaktari na wauguzi wapo.

Alisema tatizo la figo linazidi kuongezeka nchini kutokana na kuwapo ugonjwa wa kisukari na nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara zina changamoto ya kuwapo tatizo la Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi, maradhi yenye ukaribu na tatizo la figo.

Rais wa Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Figo, Dk. Onesmo Kisanga alisema chama chao kinatambua mchango unaotolewa na serikali katika kuhakikisha tiba sahihi ya masuala ya figo inatolewa kwa wananchi.

Alisema lengo lao ni kuona tiba ya figo inawafikia wagonjwa ambao wamejitokeza katika kupata matibabu ya figo kutoka kwa wataalamu wa sekta hiyo.

Aliwapongeza waandaaji wa kongamano hilo ambalo limeshirikisha madaktari na wauguzi kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambao wote watashiriki mada, ikiwamo kubadilishana utalaamu kuhusu tiba hizo.

Aliwasisitiza kuendeleza jitihada za utoaji huduma za magonjwa ya figo ambazo awali zilikuwa zinatolewa nje ya nchi.

# Jamhuri kuandaa taarifa Korti Kuu kesi wafanyakazi 15 jiji Dar

**Na Mwadishi Wetu**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya wafanyakazi 15 wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, wanaotuhumiwa kuisababishia mamlaka hiyo hasara ya Sh. bilioni 8.9, umedai kuwa uko katika hatua za mwisho za kuandaa taarifa ya kuipeleka Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Wafanyakazi hao ambao wanawakilishwa na zaidi ya mawakili 10, wanashtakiwa kwa makosa 143 ayakiwamo kuongoza genge la uhalifu, matumizi mabaya ya madaraka, kuingiza taarifa za uongo kwenye mfumo, ufujaji na ubadhirifu, kughushi, utakatishaji fedha na kusababisha hasara.

Jamhuri ilitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Pamela Mazengo wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Kutokana na maelezo hayo, Hakimu Mazengo aliahirisha kesi hiyo hadi Desemba 21, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Jopo la mawakili wa utetezi likiongozwa na Wakili Joseph Mabula, halikuwa na pingamizi.

Washtakiwa hao ni Ofisa Mtendaji wa Kata, Khalid Nyakamande (34), Ofisa Afya Patrick Chibwana (40), Karani wa Fedha, Judica Ngowo (51), Tulusubya Kamalamo (53), James Bangu (57) na Mohamed Khais (41).

Wengine ni Abdallah Mlwale (52), Deogratias Lutaza (55), Febronia Nangwa (44), Grory Eugen (46), Said Bakari (37), Josephine Sandewe (48), Dorica Gwichala (45), Jesca Lugonzibwa (53) na Ally Baruani (38), wote wakazi wa Dar es Salaam.

Ilidaiwa kuwa Julai Mosi, 2019 na Juni 30, 2021 washtakiwa wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. bilioni 8.9.

Katika shitaka la matumizi ya madaraka, washtakiwa wote 15 wakiwa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwa nyadhifa mbalimbali, walidaiwa kushindwa kuingiza mapato katika akaunti za NMB, CRDB, NBC na DCB zinazomilikiwa na jiji, hivyo kusababisha hasara ya Sh 8,931,598,500.

Kuhusu kuingiza taarifa za udanganyifu kwenye mfumo, ilidaiwa kuwa Ngowo, Nangwa na Bakari walitenda kosa hilo kati ya Julai Mosi, 2019 na Juni 30, 2021. Shtaka la ufujaji na ubadhilifu, ilidaiwa kuwa Kamalamo, Bangu, Khais, Mlwale, Lutaza, Ngowo, Nangwa, Eugen, Bakari, Sandewa na Lugonzibwa walitumia fedha za halmashauri hiyo kwa maslahi binafsi.

Kwa shtaka la kughushi linawakabili Kamalamo, Bangu, Sandewa, Gwichala, Lugonzibwa, Chibwana, Baruani na Nyakamande.

Katika shtaka la utakatishaji fedha, washitakiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo Julai Mosi, 2019 wakiwa ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kuisababishia hasara mamlaka husika Sh. bilioni 8.9.

Washitakiwa baada ya kusomewa mashitaka, hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

# Waliopinga kuondolewa maeneo yao Unguja wasikilizwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WANANCHI katika Vijiji vya Ubunji na Kajengwa Mkoa wa Kusini Unguja, wamesema haikuwa muafaka serikali kutaka kuwaondoa kwenye maeneo yao kupisha mradi wa uchimbaji wa kifusi wakati maisha yao yanategemea shughuli za kilimo.

Walisema hayo jana walipokuwa wakizungumza na waandishi wa habari katika Kijiji cha Umbuji baada ya mashamba yao kuvamiwa na kupimwa, huku kila mmoja akitakiwa kuhesabu miti ya mazao katika shamba.

Rashid Zuberi Juma, alisema maisha yao wanategemea shughuli za kilimo na mazao ya viungo na nafaka.

"Walianza kuja watu wakidai wanatoka serikalini na kuanza kupima maeneo yetu ya kilimo bila ya kutueleza kitu gani kinachotaka kufanyika na waliporudi mara ya pili walitaka tuanze kuhesabu miti ya mazao na kujiandaa kuondoka bila ya kutueleza tutakwenda kuishi wapi," alihoji.

Mkulima wa kijji hicho, Patima Vua Hassan, alisema hekaheka za kupima maeneo ya mashamba yao zilianza kufanyika Agosti, mwaka huu, bila ya kushirikishwa wala kuelezwa kitu kinachotaka kufanyika na viongozi wa Wilaya ya Kati Unguja.

"Wakati Rais anataka watu kujiajiri na kujenga masoko ya kisasa inakuaje leo miti ya mazao tuliyopanda zaidi ya miaka 20 inatakiwa kukatwa na sisi kuondoshwa jambo hili litatuongezea umaskini na kufufua maradhi," alisema Patima.

Patima mwenye watoto 12, alisema watoto wake wawili pekee ndio wenye elimu ya sekondari na akitegemea kilimo kwa ajili ya kuendesha maisha ya familia yake na kuiomba serikali kuangalia upya mpango wa kutaka kuwaondoa katika maeneo yao kijijini.

Rashid Ali Muhammed, askari mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, alisema kwa zaidi ya miaka 40 anaishi kwa kutegemea kilimo na familia yake na kushangazwa na mpango wa kutaka kufukuzwa katika maeneo yao ya asili bila kuelezwa watakapoenda kuishi na wapi watafanya shughuli zao.

Hidaya Abdallah Kheri, alisema hawapo tayari kuondoka katika mashamba yao na kumuomba Rais wa Zanzibar kusitisha mpango wa kuwafukuza.

Aidha, alisema tathmini ya miti iliyofanywa katika maeneo yao imejaa ubabaishaji na haiwezekani mti wa mdimu, mnazi au mwembe ulipwe kwa Sh. 5,000 wakati uzalishaji wa miti hiyo kwa mwaka humuingizia zaidi ya Shilingi milioni tano.

Shekha wa Kijiji cha Umbuji, Muhammadi Kassim, alikiri kuwapo mgogoro kati ya wanavijiji wa Umbuji na serikali baada ya kutakiwa kuhesabu miti ya mazao yao kabla ya kutakiwa kuondoka katika makazi yao.

Hata hivyo, alisema baada ya wananchi kuja na msimamo wa pamoja viongozi wa wilaya walifika hivi karibuni na kutoa taarifa kwamba mpango huo umesitishwa na kuwataka wawe watulivu na kuendelea na shughuli zao za uzalishaji.

"Mimi mwenyewe ni muathirika wa mgogoro huu, lakini viongozi wakiwamo mkuu wa wilaya na mkuu wa usalama wa wilaya walifika na sasa mpango huo haupo tena, serikali inaangalia uwezekano wa kuchimba kifusi katika Kijiji cha Uroa mkoani humo," alisema.

# REA yataja vikwazo kukamilisha miradi kwa wakati

**Na Zanura Mollel**

MKURUGENZI wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Injinia Jones Olotu, amesema kukosekana kwa miundombinu rafiki ya barabara kumechangia kuchelewa kwa ukamilikaji wa miradi kwa wakati katika maeneo mbalimbali nchini.

"Unakuta mradi wa kukamilika wiki moja inachukua muda hadi kufikia wiki nne, hakuna mazingira rafiki ya kufikisha vifaa, wakati mwingine hakuna madaraja tunalazimika kutumia gogo kuvuka upande wa pili na safari inakuwa ya kilomita sita kwa kuwa gari haliwezi kufika."

Akizungumza na wahariri na waandishi wa vyombo vya habari jana jijini Dar es Salaam, Olutu alisema sababu nyingine ni mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 baada ya nchi ya India na China kuingia karantini ilichangia kukosekana kwa malighafi ya vifaa vya umeme na kusababisha miradi ilisimama kwa muda.

Alisema hayo ikiwa ni utaratibu aliouweka Msajili wa Hazina wa kuziagiza taasisi za serikali kutoa taarifa za utendaji zao kwa wananchi kupitia vyombo vya habari.

Pia, alisema uharibifu wa miundombinu ya umeme unaofanywa na wananchi na kusababisha hasara kwa serikali, ikiwamo wizi wa nyaya za umeme na uchomaji moto nguzo za umeme.

"Kuna wananchi wanachoma moto nguzo za umeme kwa kujua au kutokujua, wengine wakati wa uandaaji wa mashamba kwa kuchoma moto na kusababisha gharama kubwa ya kuanza usimikaji upya," alisema Olotu.

Katika hatua nyingine alifafanua kuwa gharama za kuunganishiwa umeme wa REA ni Sh. 27000 na kuwataka wananchi kuepuka na vishoka wanaotumia nafasi hiyo kuwalipisha gharama zaidi.

Katika utekelezaji wa miradi ya usambazaji umeme vijijini alisema vijiji 10,127 vimepata umeme sawa na asilimia 82.21 huku vitongoji ikiwa 28,659 sawa na asilimia 44.25, matarajio ikiwa ifikapo Juni 2024 usambazaji umeme vijijini uwe umekamilika.

Aidha, alisema vijiji 2,191 miradi ya usambazaji umeme unaendelea, huku vitongoji 36,101 vikiwa bado havijafikiwa na umeme, hata hivyo Sh. trilioni 6.7 zinahitajika ili kufikisha umeme katika vitongoji hivyo.

Mkurugenzi wa Technolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala, Injinia Advera Mwijage, alisema utafiti uliofanywa na Begen Africa (PTY) mwaka 2018/2019 kupitia ufadhili wa Serikali ya Sweden, Shirika la Maendeleo la Sida na Benki ya Dunia (WB) ulibainisha kuwa kuna visiwa 196 ambavyo 143 vina makazi ya kudumu, 53 havina makazi ya Kudumu.

Alisema pamoja na changamoto kufika katika maeneo ya visiwani husuani katika ukanda wa pwani wenye unyevunyevu (delta), serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya kuhakikisha kila Mtanzania aliyepo eneo la vijiji-mji na vijijini wanafikiwa na huduma, visiwa 72 kati ya 143 ambavyo vina makazi ya kudumu vimepata umeme.

Hata hivyo, alisema visiwa 28 vitapelekewa umeme, mradi huo unatekelezwa na sekta binafsi na taratibu zingine zimekwishaanza ikiwamo kazi za upembuzi yakinifu, mpango wa biashara, vyeti vya athari za mazingira zinaendelea ili mradi uanze kutekelezwa. "Miradi hii itakwenda kubadilisha maisha ya wananchi kwa kutunza mazingira kwa kuwa watapatiwa majiko banifu yenye kutumia kuni chache pamoja na mkaa kidogo."

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri (TEF), Deodatus Balile aliishauri REA kutumia fursa ya kupeleka bomba la gesi Kanda ya Ziwa ikiwa ni sehemu ya kujipatia kipato na kuepuka kutegemea ruzuku pekee.

"Pia tengeni bajeti kwa ajili ya kufanya vipindi na kuandaa makala mbalimbali katika vyombo vya habari ili wananchi waweze kutambua miradi inayotekelezwa pamoja na kupata elimu, niwapongeze kwa kazi nzuri, ukitembea vijijini unakuta nguzo za umeme zimefika."

# UVCCM yakabidhi vifaa vya TEHAMA vyuoni

**Na Maulid Mmbaga**

MAKAMU Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Rehema Sombi, amekabidhi vifaa mbalimbali vya kiofisi na TEHAMA kwa seneti ya vyuo na vyuo vikuu nchini kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi wao.

Vifaa hivyo ambavyo thamani yake haikutajwa kwa sababu maalum, vilivyowasilishwa katika vyuo ikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM), Chuo cha Uhasibu (TIA) cha Arusha na Singida, chuo cha Rukwa na Chuo Kikuu cha St. John's (SJUT) cha Dodoma.

Akikabidhi vifaa hivyo jana mkoani Dar es Salaam, Rehema aliahidi umoja huo utaendelea kuwaunga mkono vijana wote wanaokiunga mkono chama hicho katika kukiletea maendeleo na utekelezaji wa ilani yake ya uchaguzi.

Rehema alisema umoja huo una wajibu wa kuongoza shughuli zinazohusu maendeleo na maslahi ya vijana nchini, huku akiwasisitiza waliopata fursa ya elimu katika ngazi za vyuo vikuu na taasisi mbalimbali kuhakikisha wanasoma kwa bidii na kuwa na maarifa makubwa.

"Nimeendelea kufanya juhudi za kuhakikisha ninawaona wadau wa maendeleo. Naushukuru Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu wake, Justina Mashiba, kwa kuonesha nia na kutoa mchango katika kugusa wanafunzi na elimu ya juu na kutupatia vifaa hivi ambavyo leo (jana) ninaviwasilisha.

"Shabaha ya chama kuunda umoja wa vijana ni ili kuwa shule ya kuandaa wanachama safi, viongozi bora na imara. Hivyo, kwa sababu hiyo UVCCM inaendelea kuandaa vijana kuwa raia wema kwa taifa letu na chombo hiki ni sawa na tanuri la kuoka makada wazuri wanaounga mkono sera, siasa na itikadi za chama," alisema.

Alieleza kuwa kutokana na msingi huo ndio maana zilianzishwa seneti za vyuo vikuu za UVCCM, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwatambua vijana waliokubali kuishi kwa kuzingatia misingi ya taifa na wenye vipawa na kuwaandaa kuwatumikia wananchi.

Alisisitiza UVCCM itaendelea kuwa kamisaa wa kuhakikisha inatambua mchango wa vijana wanaounga mkono juhudi za chama walioko vyuo vikuu kupitia seneti na kuwa daraja la kuwaunganisha na wananchi katika ujenzi wa maendeleo ya taifa.


Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

## EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the strategic business needs which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the following positions: -

**1. POSITION: CAPTAIN - (30 POSTS)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have flown with more than 3500 flying hours with an Airline Transport Pilot License, Multi Engine and Instrument Rating.
- Must have 1000 hours as a Pilot in Command and an experience of handling a minimum of 20 tons equipment or above with a good performance.

**1.2.DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Responsible for safety of the aircraft, its occupants and cargo pre, during and post flight.
- Maintain a high standard of discipline, appearance, uniformity and promptness of Co-pilots and Cabin Crew.
- Determine the achievement of commercial aspects of flights safety is not impaired to obtain additional revenue load for the Company.
- Ascertain that Flight Plans, Notam, Fleet Notices, Weather and any pertinent documentation and service items that flight may require are briefed.
- Verify that the loading of aircraft being performed in accordance with laid down procedures.
- Report all incidents and accidents.
- Verify that all documents/certificates required being on board the aircraft are available and valid.
- Report any Flight delays of flights.
- Accept and sign for diplomatic mail, precious cargo and supervise stowage aboard the aircraft and handover to destinations.
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**2. POSITION: FIRST OFFICER - (26 POSTS)**

**2.1.MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have flown with more than 250 flying hours or above with Commercial Pilot License, Multi Engine with Instrument Rating.
- Must be with an experience of handling a minimum of 10 tons' equipment with good performance.

**2.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- To participate in the Pilot-in-Command's crew briefing, and make himself aware of all relevant aeronautical and meteorological information as well as relevant papers documenting the aircraft technical status and its anticipated load.
- To prepare the OFP and when necessary, file the ATS Flight Plan with the appropriate Authority. If stored plans are used then he should ensure that the correct plan has been activated
- To carry out such duties concerning the flight in accordance with the SOP, including procedures, limitations and performance related to the specific aircraft type, as allocated to him by the Pilot-in-Command;
- To confirm the safe navigation of the aircraft, maintaining a continuous and independent check upon both the geographical position of the aircraft and its safe terrain clearance
- To safely and properly conduct the flight in compliance with the current flight plan and the Pilot-in-Command's instructions when the Pilot-in-Command is not at the controls. Any change to the current flight plan has to be notified to the Pilot-in Command.
- To provide advice, information and assistance to the Pilot-in-Command, as may contribute favorable towards the safe and efficient conduct of the flight.
- To assist the Pilot-in-Command in administration duties related to the flight and
- To seek and receive information and/or explanation from the Pilot-in Command, as may be necessary to enable fulfilment of functions.
- To assist the Flight Safety Department for all Technical related matters
- Perform any other official duties as may be assigned by your supervisor.

**3. TERMS AND CONDITIONS:**

Ten (10) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council-NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. Name and address of at least two reputable referees;
v. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**5. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on 24th November, 2023**

217726302

***ATCL is an equal opportunity employer. Women are encouraged to apply. Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# REA isaidiwe miundombinu rafiki kukamilisha miradi kwa wakati

**KATIKA** mafanikio inayojivunia Wakala wa Niashati Vijijini (REA) ni kusambaza huduma ya umeme katika vijiji nchini 11,213 mpaka ilipofika Novemba 22, mwaka huu.

Hata hivyo, pamoja na mafanikio hayo Wakala huyo anakutana na changamoto nyingi wakati wa utekelezaji wa kutoa huduma hiyo, ikiwamo ya miundombinu mibovu.

REA ili iweze kutekeleza jukumu lake la kusambaza umeme vijijini ni lazima iwe na vifaa vitakavyowezesha huduma hiyo kuwafikia wananchi. Kifaa muhimu ni nguzo ambazo huhitajika kusimikwa ili nyaya za umeme ziweze kupita na kuingizwa kwenye nyumba.

Changamoto wanayokutana nayo ni miundombinu ya usafirishaji katika baadhi ya vijiji kutokuwa rafiki na hivyo kuwalazimu kutumia muda mrefu kukamilisha mradi kwa sababu ya usafirishaji wake kuwa mgumu.

Vilevile, mahitaji ya huduma kuwa makubwa kuliko uwezo wa REA na hivyo kuwapo kwa malalamiko ya ucheleweshaji wa kupata huduma hiyo.

Kama kutakuwa na miundombinu mizuri ya barabara za kusafirishia vifaa hivyo, mradi huo ungekuwa unakwenda haraka na wananchi wakapata huduma kwa wakati na kuondoa malalamiko.

Kazi kubwa ya REA ni kusambaza huduma ya umeme vijijini na mafanikio yanaonekana baada ya maeneo mengi ya vijijini hivi sasa kuwa na nishati hiyo.

Maendeleo yanaonekana kwa kuwa vijijini sasa hivi zinapatikana huduma zote ambazo hapo awali ilikuwa mpaka zifuatwe mijini.

Vijana wengi wamejitengenezea ajira ikiwamo kuwa na saluni za nywele, mashine za kusaga nafaka, kufungua biashara za kuchomelea magrili ambayo kabla ya huduma ya umeme kuanza kusambazwa vijijini ilikuwa lazima mwenye nyumba achukue vipimo na kuvipeleka mjini ndipo atengenezewe.

Walengwa wa miradi inayofadhiliwa na REA ni wananchi waishio maeneo ya vijijini Tanzania Bara. Wananchi hawa ni takribani asilimia 75 ya wote wanaoishi huko wanaokadiriwa kufikia milioni 56.8.

Lengo la kuanzishwa kwa REA ni kuhamasisha, kuratibu na kuwezesha uanzishwaji na uendelezaji wa miradi ya nishati bora vijijini ili kuhakikisha kuwa nishati hiyo inachangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma za jamii.

Pia nishati hiyo inachangia katika kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa vijijini katika hali endelevu na uendelezaji wa miradi ya niashata unazingatia uhifadhi wa mazingira na usawa wa kijinsia.


Tofauti ya Shirika la Umeme Nchini (Tanesco) na REA, Shirika la Umeme linafanya biashara ya kutoa huduma ya umeme ili liweze kujiendesha, lakini REA inatoa huduma kwa wananchi kwa sababu inapata ruzuku kutoka serikalini.

Hata hivyo, taasisi hizo mbili zinashirikiana kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yao kwa kuwa lengo lao ni moja la kutoa huduma kwa wananchi.

Wakala wa Nishati Vijijini lengo lake ni kuhakikisha mpaka ifikapo Juni, mwakani vijiji vyote Tanzania Bara viwe vimepata huduma ya umeme na hilo linawezekana kama changamoto zilizoelezwa zitapatiwa ufumbuzi mapema.

Lengo kubwa la serikali ni kuona kuwa wananchi wake wote wanapata huduma ya umeme ili kila mtu aweze kuepukana na uharibifu wa mazingira wa kukata miti ovyo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na kuwaepusha wananchi maradhi yanayotokana na uvutaji wa hewa chafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera TAMWA mavuno miaka 36, mwalikwa mwenzenu Mama wa Nchi

**CHAMA** cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) kinatarajia kufanya Maadhimisho yake ya Miaka 36 Novemba 28 na 29, ndani ya Dar es Salaam.

Rais Samia Suluhu Hassan, ndiye anayetajwa kuwa ni mgeni rasmi katika maadhimisho hayo yaliyobeba mambo kadhaa, ikiwamo kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii.

Haikuwa rahisi kuanzishwa kwa taasisi hiyo binafsi. Kulikuwapo na wabeba maono waanzilishi wa TAMWA ambao ni Fatuma Alloo, Nellie Kidela, Edda Sanga, Elizabeth Marealle, Rose Kalemera, Halima Shariff, Rose Haji, Valerie Msoka, Ananilea Nkya, Pili Mtambalike, Chemi Chemponda, Leila Sheikh na Jamila Chipo.

Kikosi kazi hicho cha wanawake 13, ndiyo kilianzisha harakati za TAMWA, ambayo sasa safari yake ya miaka ya 36, ikiwa chini ya Mwenyekiti Joyce Shebe na Mkurugenzi Dk. Rose Reuben, imeendelea kufanya shughuli zake kwa kujituma.

Ikiwa na malengo kadhaa yenye manufaa kwa jamii, ikiwamo kuhamasisha upatikanaji wa haki za wanawake na watoto wa kike, kuanika ukatili uliotendwa dhidi ya watoto wa kike, ikiwamo ukeketaji, mimba za utotoni, ndoa za utotoni na uminywaji wa haki ya kupata elimu.

Ni wazi kuwa TAMWA ilibaini kukithiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, ambapo waathirika wakubwa walikuwa ni wanawake, pia walibaini uwepo wa mila potofu ikiwamo wanawake kunyimwa kumiliki ardhi kwenye baadhi ya mila na tamaduni za makabila kadhaa.

Kwa hiyo, imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa bidii na ushirikiano na taasisi nyingine husika za serikali na binafsi tangu kuanzishwa kwake mwaka 1986.

Nafikiri TAMWA inapaswa kumshukuru Mungu na washirika na wadau wake, kwa ujumla kutokana na mafanikio mazuri ambayo yataendelea kuishi ndani ya historia.

Wahenga wanasema palipo na ukweli uongo hujitenga, ni wazi kuwa kuna mwamko ndani ya jamii katika kuwaandikisha shule na ukifuatilia vizuri idadi ya wasichana, ndiyo huwa kubwa ikilinganishwa na wavulana.

Hii inamaanisha kwamba kama kusingekuwa na hamasa mbalimbali ikiwamo hizo zilizofanywa na TAMWA wasichana wengi wangeendelea kuminywa kwa kutoandikishwa shule, hivyo wangekoseshwa kuwa na wataalamu wa kutosha, taaluma mbalimbali nchini.

Nguvu za harakati zilizotumika zimezaa matunda mema yanaonekana wazi, sasa ikiwamo kuongezeka kwa idadi ya watoto wa kike wanaoanza na kumaliza elimu ya msingi na sekondari hadi elimu ya juu.

Hii ni kwa sababu jamii imepata elimu na kutambua umuhimu wa kuwaandikisha shule watoto wa jinsi zote badala ya kubagua kama walivyokuwa wanafanya awali. TAMWA yenyewe imeonyesha mfano wa kuwashirikisha wanahabari wanaume katika miradi yake kadhaa iliyoitekeleza.

Ninavyotambua ni kwamba TAMWA, imeshiriki kwenye harakati za masuala kadhaa ikiwamo kuchangia kupitishwa kwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana (SOSPA 1998).

Pia, TAMWA imeshiriki kufanikisha kuanzishwa kwa kituo cha usuluhishi (Crisis Resolving Center), kukomesha mauaji ya wanawake wazee(vikongwe), hasa mikoa ya Tabora na Shinyanga. Kufutwa kwa Sheria ya Wanawali Zanzibar.

Mengine ni kuongezeka kwa idadi ya wanawake kwenye nafasi za uongozi wa kuchaguliwa, kuanzishwa kwa Sera ya Jinsia na ya rushwa ya ngono kwa baadhi ya vyombo vya habari, kuongeza hamasa kwa jamii kuandikisha shule watoto bila ubaguzi wa jinsia, kushiriki kuzuia ndoa za utotoni na ukeketaji.

Kwa haya mafanikio, nadhani TAMWA inastahili kuendelea kuwapo kama taasisi daraja la kuvusha kutoka hatua moja kwenda nyingine, kwa kuwa imefanya juhudi za makusudi kugharamia masomo kwa baadhi ya wanahabari wanawake.

TAMWA inastahili kuendelea kuungwa mkono na washirika wake na jamii kwa ujumla, ili iendelee kutumika vyema.

## HABARI KITAIFA

# Wenye ulemavu wapatiwa vifaa saidizi

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) kwa kushirikiana na shirika la CCBRT wametoa msaada wa viti mwendo na vifaa saidizi 55 kwa watu wenye ulemavu kutoka mkoani Geita kwa lengo la kuwarahisishia kutembea na kushiriki shughuli za kijamii.

Msaada huo ulikabidhiwa juzi mjini Geita kupitia mpango maalum wa usambazaji viti mwendo. Ni mkakati wa GGML kujitolea kwa jamii na kuleta matokeo chanya kutokana na shughuli zake za uchimbaji madini.

Akikabidhi msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Terry Strong alisema kampuni imejitolea kuendelea kuzingatia utu kwa watu wote ikiwamo wadau wake na jamii wanamofanya kazi.

"Ni sehemu ya mipango kadhaa ya huduma za afya ambayo tumeifanya kwa ushirikiano na CCBRT, ambayo imekuwa inafanya kazi kwa bidii katika kutoa huduma za matibabu na urekebishaji wa viungo mbalimbali vya mwili kwa gharama nafuu na kuwawezesha watu wenye mahitaji maalum na familia zao kurejesha tabasamu.

"Tunaamini kwamba kila mtu anastahili utu, heshima, na fursa sawa za kustawi maishani. Pia tunatambua kwamba watu wanaoishi na ulemavu wanakabiliwa na changamoto nyingi na vikwazo katika kupata huduma za msingi, elimu, ajira na ushirikishwaji wa kijamii.

"Ndiyo maana tunajivunia kuunga mkono mpango huu ambao utawapa huduma zinazofaa na zilizoboreshwa ambazo zitaboresha uhuru na ubora wa maisha," alisema mkurugenzi huyo.

Mwakilishi wa CCBRT, Dk. Neophita Lukiringi aliwashukuru kampuni hiyo ya uchimbaji madini kwa kuwafikiria watu wenye ulemavu na kuwapatia viti mwendo ambavyo ni sahihi.

Alisema mtu mwenye ulemavu akipatiwa kiti mwendo ambacho si sahihi kwake, kinaweza kumletea madhara zaidi.

"Lakini GGML waliona pamoja na kuwasaidia watu wenye ulemavu hawakutaka kugawa ovyoovyo, wakafikiria tupate vifaa ambavyo vitawasaidia kweli," alisema.

Daktari huyo kutoka CCBRT alisema mtu mwenye ulemavu akipatiwa kiti mwendo kisicho sahihi kinaweza kumsababisha apinde mgongo, kifupishe misuli yake na kumwongezea ulemavu zaidi.

"Ninatoa wito kwa Watanzania ambao wanapenda kusaidia watu wenye ulemavu wasitoe viti mwendo bila kutafuta wataalamu wa kushirikiana nao kwa sababu hata Shirika la Afya Duniani (WHO) linasisitiza viti mwendo vitolewe na watu waliofunzwa ili kukabili madhara hayo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Kanali Boniphace Maghembe ambaye pia alikuwa mgeni rasmi katika hafla ya makabidhiano hayo, aliwapongeza GGML kwa kuendelea kuijali jamii ya watu wanaouzunguka mgodi huo.

Pia aliipongeza CCBRT kwa kuungana na GGML kutoa elimu ya kitaalamu kuhusu matumizi sahihi na kutoa ushauri sahihi wa vifaa hivyo vya watu wenye ulemavu.

Mmoja wa wanufaika wa msaada huo, Matendo Sitta alishukuru GGML na CCBRT kwa moyo wa upendo walioonesha na kuwapatia viti mwendo ambavyo sasa vitawasaidia kuchangamana na jamii.

"Tunaomba msiishie kwetu kwa sababu kuna wenzetu wengi wenye changamoto, hivyo tunaomba waendelee kuwa na moyo wa utoaji kwa sababu sasa hivi tunaweza kwenda hata kwa jirani kupiga stori na tunaahidi kutunza vyombo hivi," alisema.



Mkuu wa Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Prof. Shadrack Mwakalila akizungumza katika kongamano la kusanyiko la wahitimu waliosoma katika chuo hicho, Kigamboni Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbarawa ashtushwa timuatimua, uhamisho holela watumishi TASAC

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa ameeleza kuchukizwa na tabia ya viongozi wa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) kufukuza na kuwahamisha ovyo watumishi, akionya kuwa ni chanzo cha shirika hilo kukosa ufanisi kiutendaji. Amesema shirika hilo tangu lilipoanzishwa mwaka 2018 limekuwa haliendelei wala kuleta tija serikalini kutokana na baadhi ya viongozi wenye tabia ya kufukuza na kuhamisha watumishi ovyo pasi na sababu yoyote.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na wafanyakazi wa taasisi hiyo, kikao kilichokuwa na lengo la kusikiliza kero na kuweka mikakati ya kuliendeleza shirika hilo.

"Hili shirika kila siku ni malalamiko, hii simu yangu imejaa meseji za malalamiko. Mna nini ninyi? Sasa nimekuja hapa kuwaeleza kuwa mliokuwa mnajifanya miungu watu muda wenu umefika. Mtaondoka! Ninarudia mtaondoka," alionya.

Prof. Mbarawa alisema anachohitaji TASAC ni nidhamu na kufanya kazi kwa malengo ya kulifikisha shirika hilo sehemu sahihi.

"Wewe unayefukuza watu ni bora wewe uondoke, taasisi ibaki. TASAC hakuna mradi wowote unaoendelezwa, kila siku mnafukuzana tu. Hakuna watu wanaoendelezwa kimasomo, lazima staili yenu ya kuongoza ibadilike. Tunataka miradi ya kidijitali ikamilike na si malalamiko kila siku."

Alimwagiza Mkurugenzi wa TASAC, Mohamed Salum kuweka utaratibu wa kukutana na wafanyakazi kila wakati ili kusikiliza na kutatua matatizo yanayowasibu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TASAC, Mussa Mandia, alisema: "Tumepokea maelekezo yako (waziri), tunakuahidi ndani ya muda mfupi utaona mabadiliko kwa sababu hayo uliyoyasema ni kweli yapo na hata mimi jana (juzi) usiku nimepokea malalamiko mengi sana".

# Majaliwa apongeza mikakati kuongeza ujumuishi kifedha

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amevutiwa na jitihada zinazofanywa na Benki ya Exim Tanzania kujitanua na kusogeza huduma zake karibu zaidi kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Ameitaja ni hatua itakayosaidia kukuza uchumi wa maeneo na kuimarisha utangamano wa kijamii.

Waziri Mkuu alitoa pongezi hizo juzi alipotembelea banda la maonesho la benki hiyo muda mfupi kabla ya kufungua maadhimisho ya Wiki ya Huduma ya Fedha yanayoendelea kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini hapa.

Benki hiyo ni moja ya wadau muhimu wa maonesho hayo yanayotarajiwa kuhitimishwa Jumapili.

Akiwa kwenye banda hilo, Waziri Mkuu alipatiwa maelezo kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo kutoka kwa Meneja Masoko na Mawasiliano, Kauthar D'Souza ambaye pamoja na kuelezea baadhi ya huduma za kifedha wanazotoa, pia alibainisha mkakati wao katika kujitanua maeneo mbalimbali nchini.


"Niwapongeze sana kwa jitihada mnazoendelea kuzifanya katika kupanua zaidi huduma zenu, hata hivyo jitihada zaidi zinahitajika ili hizi huduma nzuri mnazoendelea kuzitoa ziwafikie wananchi wengi zaidi hususani waliopo pembezoni huko ambao bado hawajafikiwa na huduma rasmi za kifedha," Waziri Mkuu alisema.

Alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa watoa huduma za kifedha nchini kuhakikisha wanaendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma na kupunguza gharama za uendeshaji huduma hizo zikiwAmo riba na ada ili wananchi wengi watumie huduma za fedha zilizo rasmi.

Kauthar alibainisha kuwa benki hiyo sasa ina mtandao wa matawi 33 na mawakala 1,500 nchi nzima. Mkakati wake ni kuwekeza zaidi katika utoaji huduma kupitia ubunifu wa kidijitali ili kutoa masuluhisho ya kibenki yanayofaa na salama kwa wateja wake.

"Pia tunatambua wajibu tulionao katika kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi hapa nchini na ndio sababu moja ya kipaumbele chetu ni kuwawezesha watu binafsi na wafanyabiashara wakiwamo wanawake na wajasiriamali kupitia huduma zetu mahususi kwa ajili yao ikiwamo akauti ya Wajasiriamali pamoja na akaunti iliyobuniwa kwa ajili ya wanawake wanaopambana kukuza mitaji ya biashara zao," alisema.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**



# Upasuaji mkubwa JKCI waokoa milioni 500/-

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na Open Heart International, wamefanya upasuaji mkubwa na wa kwanza nchini kwa wagonjwa 11 wakiwamo ambao mishipa yao ilipasuka kutokana na presha, ikiokoa Sh. milioni 500.

Upasuaji huo wa moyo ambao umelenga kuwafanyia wagonjwa 16, tayari umefanywa kwa wagonjwa 11 wakiwamo watoto na watu wazima, huku gharama za matibabu kwa wagonjwa hao yangefanyika nje ya nchi yangegharimu Sh. milioni 60 kwa mgonjwa. Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, akifafanua kuwa wataalam 23 kutoka taasisi hiyo ya Australia wametoa matibabu, kuwaongezea ujuzi Watanzania. Upasuaji wa aina hiyo ulikuwa haujafanyika nchini.

"Kwa wiki moja taasisi hii imepata wageni 23 kutoka Australia. Wamo wateknolojia tiba, wauguzi, madaktari bingwa wa upasuaji moyo na watoto.

"Huu upasuaji huu ni kwa mshipa mkubwa wa moyo unaopeleka damu sehemu mbalimbali, tulikuwa hatufanyi. Awali tuliwapeleka India kwa Sh. milioni 60 kwa mgonjwa.

"Ila wamekuja kutufundisha kufanya upasuaji huu na tutaanza kufanya na gharama nchini itakuwa Sh. milioni 20 kwa mgonjwa. Matibabu haya yakifanyika kwa mshipa mkubwa uliopasuka ni muhimu kwa sababu unapeleka damu sehemu tofauti mwilini," alisema Dk. Kisenge.

"Ulaji usiofuata lishe, mafuta kuziba katika mishipa, kutofanya mazoezi kunaongeza uzito na kufanya mtu kupata presha na mishipa kupasuka, hivi sasa kuna ongezeko la asilimia 25 la ugonjwa wa presha, hata vijana. Tunatoa elimu, ili kujikinga.

"Kwa uwezo wa matibabu ya kibingwa ya JKCI hatukosi kuwataka washirika wetu ikiwamo Open Heart International ambao tupo nao tangu mwaka 2015. Kutokana na uwezo huu kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita tumepokea wagonjwa 60 kutoka nje kama Ufaransa.

"Wagonjwa wametoka visiwa vya Comoro, Malawi, Msumbiji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zimbabwe na imetushangaza wengine kutoka Ufaransa na Ujerumani. Hii ni sehemu ya tiba utalii, itaongeza mapato na fedha za kigeni," alisema Dk. Kisenge.

Dk. Darren Wolfers, Mratibu wa Miradi kutoka Open Heart International, alisema kuwapo vifaa tiba na rasilimali watu katika taasisi hiyo, kunaifanya kuwa kivutio kwa wageni kutoka nje hususan katika mafunzo na matibabu.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba (kushoto), wakati akitoa taarifa ya mfuko katika Maadhimisho ya 3 ya Wiki ya Huduma ya Fedha Kitaifa, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha juzi. Wengine ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako (kulia), Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Mhandisi Cyprian Luhemeja (wa pili kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Zitto asuka mkakati kuibana serikali ubovu wa barabara

**Na Julieth Mkireri,** KIGOMA

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe amesema chama hicho kitaanza kampeni maalum ya kuilazimisha serikali kujenga barabara ya Simbo-Mpanda ili kuondoa kero ya usafiri kwa wananchi.

Amesema atakutana na Waziri wa Ujenzi na Waziri wa Fedha kwa lengo la kuwasilisha hoja hiyo ili barabara hiyo ya kimkakati ijengwe haraka kwa kiwango cha lami.

"Sasa tunaanza kampeni maalum kama ambavyo maeneo mengine barabara zinajengwa kwa utaratibu wa mkandarasi kujenga kwa fedha zake kwanza na baadaye kulipwa kwa awamu ili kuondokana na kero ya usafiri kwa wakazi wa maeneo hayo," alisema Zitto.

Alieleza hayo jana alipohutubia wananchi katika Kijiji cha Lukoma, Kigoma Kusini katika ziara yake ya kukijenga chama kwa kuzungumza na wananchi na viongozi wa chama hicho kuanzia ngazi ya kijiji. "Nimeuliza nimeambiwa watu wanalipa Sh. 25,000 kwa basi kutoka Kaliua mpaka mjini Kigoma, maana yake ni kwamba maskini anakandamizwa zaidi kutokana na miundombinu mibovu ya barabara.

"Miundombinu inamfanya maskini aendelee kuwa maskini kwa kulipia gharama kubwa kwenye huduma na bidhaa anazopata. Kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya miundombinu na umaskini.

Haiwezekani mfuko wa saruji uuzwe kwa Sh. 30,000 hapa ambayo ni mara mbili ya bei ya Dar es Salaam," alifafanua.

Zitto alisema kwa kuwa barabara hiyo ni ya kimkakati na inaweza kutumika katika masuala ya kiusalama, ni vyema serikali ikafikiria namna ya kuijenga kwa haraka na kuwarahisishia wananchi usafiri wa kufika maeneo mengine.

Alisema chama hicho kitaendelea kuhakikisha mpango wa matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo ya vijiji unazingatiwa kuepusha migogoro inayotokea kila wakati.

Alisema wataendelea kuwasaidia wananchi kwenye maeneo yenye migogoro ili itatuliwe kwa haraka waendelee kufanya shughuli zao za kilimo.

Vilevile, alisema wakazi wa Mkoa wa Kigoma wanatakiwa kufanya mabadiliko katika uchaguzi ujao kwa kuwachagua wawakilishi kutoka chama hicho ili wakawatetee na kuwaletea maendeleo

Alisema kukosekana kwa wawakilishi kutoka chama hicho ni sababu ya "udumavu wa maendeleo" kwa kuwa kwa kipindi kifupi baadhi ya majimbo yaliyoongozwa na vyama vya upinzani mabadiliko yalianza kuonekana kwa jitihada walizokuwa wanazifanya za kuusemea mkoa huo kwenye vyombo vya uamuzi.

# ATCL kushusha Boeing MAX na Dreamliner mwakani

**Na Joseph Mwendapole**

WAKATI Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ikitarajia kupokea ndege nyingine aina Boeing 737 MAX Januari mwakani, serikali imelitaka shirika hilo kuongeza ubunifu na mikakati itakayoondoa malalamiko ya wateja ya kuahirisha safari.

Mbali na ndege hiyo itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 189, ATCL pia inatarajia mwezi Machi mwakani kupokea ndege nyingine kubwa aina ya Dreamliner 787-800 itakayokuwa na uwezo wa kubeba abiria 260.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alipotembelea ofisi za shirika.

Alisema tabia ya kuahirisha safari ilikuwa inafanyika kwa kisingizio cha upungufu wa ndege, lakini baada ya ujio wa ndege hizo mbili mwakani shirika litakuwa na ndege 16.

"Tumetoka kwenye ndege moja mpaka mwakani tutakuwa na jumla ya ndege 16. Hivyo, yale malalamiko ya wateja ya kuahirisha safari hatutaki kuyasikia tena kwa sababu ndege mnazo za kutosha na marubani 105.

"Changamoto kubwa ya kuahirisha safari ilikuwa sababu ya uchache wa ndege ndiyo maana serikali inanunua ndege zingine, lakini na ninyi mkae chini mje na mpango mkakati mzuri wa namna ya kuhakikisha habari ya kuahirishaahirisha safari inafika mwisho," alielekeza.

Kihenzile alisema kuwa miaka ya nyuma shirika hilo lilikuwa likipata hasara ya Sh. bilioni 170, sasa analipongeza kwa kuendelea kupunguza hasara mwaka hadi mwaka na kwa hesabu za mwaka huu inaonyehsa kwamba litapata faida ya bilioni 1.5.

Alisema ATCL ilikuwa ikidaiwa Sh. bilioni 236 lakini mpaka sasa asilimia 60 ya madeni hayo yameshalipwa na alilitaka shirika kutumia fursa hiyo kuboresho huduma zake na kujiendesha bila kutegemea ruzuku ya serikali.

"Mkurugenzi ameaniambia kwamba mnajiendesha kwa asilimia 99.6, ninawapongeza sana kwa hatua hii kubwa mliyofikia kwa sababu serikali kazi yake ni kuwekeza tu, masuala ya mishahara na uendeshaji wa shughuli za kila siku mjitegemee na serikali itajisikia faraja kuona mnajitegemea kwa asilimia 100," alisema.

Aliutaka uongozi wa ATCL kuwa na mikakati ya ubunifu ya kuhakikisha shirika hilo linajiendesha kibiashara na kwa faida kwa kuiga mikakati ambayo imefanywa na mashirika mengine yaliyopiga hatua kubwa kwenye biashara ya usafiri wa anga.

"Kama wenzetu KQ wamefika pale sisi tunashindwa nini kufika walikofika wenzetu? Wekeni mipango ya muda mrefu, mfupi na wa kati na serikali ingependa kuona ATCL linakuwa shirika kubwa lenye nguvu kwenye ukanda huu," alisema Kihenzile.

Alisema idadi ya wawekezaji wanaokuja kuwekeza nchini imekuwa inaongezeka kwa kasi kubwa, hali ambayo inaonesha kuwa mahitaji ya usafiri wa ndege nayo yataongezeka kutokana na safari za wawekezaji hao.

Pia, alilitaka shirika hilo kufanyia kazi ipasavyo hoja zote za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kupanga hesabu vizuri. Wizara haitapenda kuona taasisi zake zinakuwa na hesabu zenye shaka.

Vilevile, Naibu Waziri alieleza kushangazwa na tabia ya watu kukata tiketi na kuacha kusafiri, hali ambayo alisema inawanyima fursa watu wengine waliokuwa na nia ya kusafiri kwenda kwenye majukumu mbalimbali.

"Hili limenishangaza sana, unaingia kwenye mtandao unaona tiketi zimejaa, lakini ukibahatisha ukapata tiketi ukaingia kwenye ndege unakuta viti vingi viko tupu. Takwimu nilizopewa kuanzia Agosti, Septemba na Oktoba mwaka huu watu 37,992 walikata tiketi, lakini kati ya hao, 1,103 hawakusafiri. Sasa fikiria ulivyozuia nafasi za watu kusafiri," alifafanua.

Mkurugenzi Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi alisema kuwa Januari mwakani wanatarajia kupokea ndege moja aina ya Boeing na mwezi Macji watapokea ndege nyingine aina ya Dreamliner.

Alisema, wamejitahidi kupunguza hasara kutoka Sh. bilioni 170 kwa mwaka na hesabu za mwisho zilizokaguliwa walikuwa na hasara ya Sh. bilioni 33 lakini kwa hesabu ambazo hazijakaguliwa za mwaka 2022/23 inaonesha watakuwa na faida ya Sh. bilioni 1.5.





Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba (wa pili kulia), akizungumza na baadhi ya wajasiriamali wanawake wanufaika wa Programu ya Uwezeshaji Wanawake (WEP) ya Benki ya Exim, alipotembelea banda la maonyesho la benki hiyo, katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UNICEF yataka dhamira ya pamoja kunusuru watoto

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

MWAKILISHI Mkazi wa UNICEF nchini, Elke Wisch ametoa wito kwa wadau wa watoto duniani kuweka upya dhamira ya pamoja kwa ustawi na ustahimilivu wa watoto wa siku zijazo.

Amesema dhamira ya pamoja inapaswa katika kukabiliana na changamoto zinazoongezeka za mabadiliko ya hali ya hewa, athari za mazingira na maafa ya asili.

Jijini Arusha juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Haki ya Mtoto, Elke alisema kila mmoja anapaswa kujua mabadiliko ya hali ya hewa, uchafuzi wa mazingira na upotezaji anuawai vimeunda shida ya sayari ambayo inaathiri si tu mustakabali wa sayari na ubinadamu, bali maisha ya kila siku na utambuzi wa haki.

"Mamilioni ya watoto duniani kote ikiwamo hapa Tanzania, wanaathiriwa na mabadiliko haya. Haki zinazotokana na kanuni za kutobagua, maslahi bora ya mtoto na heshima kwa maoni ya watoto huwa muhimu zaidi katika muktadha wa mabadiliko ya hali ya hewa," alisema.

Aliongeza kuwa kanuni ya kutomwacha mtu nyuma na kutomwacha mtoto nyuma, inachukuliwa kwa uzito wakati wa kuzingatia athari za mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa kwenye sayari ya watu na hasa watoto walio na miaka 10 inayojumuisha watoto wa kizazi kipya.

Alisema wote wana uwezo mkubwa wa kuwa na nguvu ya mabadiliko chanya, mradi tu jamii inawekeza katika ujasiri na uwezeshaji watoto na vijana kwa kutambua haki ya afya, lishe, elimu na ulinzi.

"Ninaipongeza Serikali ya Tanzania kwa kutetea haki za watoto zinazoleta maendeleo na matokeo katika mtoto kama afya, lishe, ujuzi wa elimu, na ulinzi wa mtoto.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuipongeza serikali kwa hatua iliyofikiwa katika viashiria vyote vya maendeleo ya mtoto baada ya kuona maendeleo makubwa yaliyopatikana kwa watoto na familia zao kote nchini," alisifu.

Alitoa wito wa kujitolea upya, kuongezeka kwa uwekezaji na hatua za kulinda maendeleo yaliyopatikana hadi sasa na kukabiliana na changamoto mbili za kutambua uwezo wa idadi ya watoto inayoongezeka wakati wa kulinda watoto kutokana na hatari zinazoongezeka.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo alisema dunia inapita katika vipindi vigumu vya mabadiliko ya tabianchi na hata sasa baharini maji yanaongezeka kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Pia mafuriko yanaingia katika nyumba za watu na pale ukame unapotokea, athari zinakwenda zaidi kwa watoto.

"Pale mifugo inapokosa chakula sababu ya ukame, lishe bora inakosekana na athari zinakwenda kwa watoto na katika uchumi nchi yetu tulipoingia katika mgawo wa umeme, hii athari kubwa inakwenda kwa watoto hasa wale njiti wanaohitaji oksijeni na wale kinamama wanaohitaji kujifungua, umeme unapokatika athari zinakwenda kwa mtoto.

"Hivyo, serikali imeweka sera za kumlinda mtoto katika nyanja mbalimbali ikiwamo katika utoaji elimu bure kuanzia shule za awali hadi sekondari na sasa tumewekeza zaidi kwenye ujenzi wa miundombinu na kutoa huduma stahiki katika afya ya mtoto na ujenzi wa vituo vya afya na hii Tanzania tumekuwa mfano Afrika," alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Amon Mpanju, alisema Tanzania imekuwa mstari wa mbele kulinda haki za watoto na kuwajengea uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia wizara hiyo.

# Bashungwa aibana TANROADS kuchelewesha usanifu barabara

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amemtaka Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuharakisha usanifu wa barabara kipande cha Km 36 kutoka Mkata hadi Kijiji cha Kwamsisi wilayani Handeni ili kuanza ujenzi wa kiwango cha lami kutatua kero kwa wananchi.

Bashungwa aliagiza hayo juzi katika Kijiji cha Kwamsisi wilayani Handeni alipokagua barabara ya Mkata-Pangani-Tanga mjini, akisema fedha za mradi wa ujenzi huo zimeshatolewa, lakini hadi sasa hakuna dalili za kuanza ujenzi. Alisema matamanio ya serikali ni kuona barabara hiyo inajengwa kwa kiwango cha lami kwa kuwa maeneo hayo yana uzalishaji mkubwa wa mazao, hasa muhogo.

Alisema serikali imetenga fedha ili wananchi wanufaike kwa kutoa mazao yao na kupeleka sokoni hasa kipindi cha mvua ambacho magari hayaingii mashambani.

"Na dhamira ya serikali, fedha hazitakiwi zikae benki, zinatakiwa ziwe kwenye utekelezaji. Kwahiyo, hili suala la usanifu wa kina linatakiwa lifanyike mara moja na kwa sababu serikali imeshaitengea fedha na kiu yake kubwa ni kuona barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami.

"Kwahiyo, wananchi wa maeneo haya, niwaombe mwendelee kumpa ushirikiano Rais wetu, tunaona kwenye mipango yake hajawaacha nyuma na mimi nimekuja kuwasukuma hawa watendaji wetu ili wafanye kazi usiku na mchana kuwatumikia wananchi wetu," alisema.

Waziri Bashungwa alibainisha kwamba mradi huo umechelewa kutokana na michakato mingi ya TANROADS, pia kutojipanga katika utendaji wao kwa kuwa tayari kuna baadhi ya maeneo miradi ya aina hiyo imekwishaanza.

"Wananchi hawa, pindi barabara hii itakapokamilika, Kwamsisi na maeneo mengine tuliyopita yatabadilika na kupata maendeleo makubwa sana, na hiyo ndiyo ahadi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Na niwaambie TANROADS wekeni jitihada ya kuhakikisha mnamaliza usanifu ndani ya muda mfupi, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ili wananchi hawa wapate matunda ya jitihada nzuri za serikali," aliagiza.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mohamed Besta alisema watahakikisha wanatekeleza usanifu wa kina kufikia mwezi ujao.

"Mheshimiwa waziri, ninaahidi kwamba zoezi la kumpata msanifu wa barabara hii litakuwa limekamilika kufikia tarehe 31 mwezi Desemba mwaka huu na kazi ya usanifu itaendelea.

"Ninapenda niwatoe wasiwasi wananchi wa eneo hili kwamba barabara hii mara baada ya kukamilika kwa usanifu, tutamtafuta mkandarasi wa kujenga kwa kuwa fedha zipo," alisema.

Baadhi ya wananchi kijijini huko walisema kwa mara ya kwanza tangu walipoambiwa barabara hiyo inajengwa hawajawahi kuona kiongozi kusimama eneo hilo na kuzungumzia maendeleo yake badala yake wanaona magari ya viongozi yakipita tu.

"Leo tumefurahi sana waziri huyu kusimama na kuongea na sisi kusikiliza kero yetu. Shida kubwa hapa ni ubovu wa barabara na hii hali ya mvua, hapa tunalima sana lakini ikifika msimu wa mvua kama hivi mazao yetu yanaozea shambani, hasara tunayopata ni kubwa mno," alilalamika Fadhil Sefu.

# RC: Marufuku ma-DED kuwakopa watumishi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, amepiga marufuku wakurugenzi wa halmashauri kuwakopa watumishi wa umma wanapofanya kazi, badala yake walipwe ili wafanye shughuli zao.

Pia ameahidi kupunguza kiwango cha utapiamlo unaowakabili watoto chini ya miaka mitano mkoani mwake.

Kiongozi huyo alitangaza hatua hizo jana alipojibu maswali ya waandishi wa habari kwenye mkutano ulioandaliwa na Ofisi ya Msemaji Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Queen alisema mkoa huo unakabiliwa na tatizo la utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano licha ya kuzalisha chakula cha kutosha.

Alisema ifikapo mwakani, utapiamlo unaowakabili watoto mkoani mwake utakuwa umepungua kama si kutokomezwa ili watoto wakue vizuri.

"Wataalam wa lishe waendelee kutoa elimu ya lishe katika vijiji kwenye wiki ya lishe ili wananchi wapate mbinu za namna ya kuandaa vyakula vya lishe kwa watoto," aliagiza.

Kuhusu watumishi wa umma wanaodai stahiki zao, Queen alielekeza wafike ofisini kwake ili wasaidiwe kupata haki zao za malipo ya likizo, ugonjwa na malipo ya muda wa kazi za ziada.

Kuhusu mila potofu, Mkuu wa Mkoa alisema zimepungua kutoka asilimia 70 mwaka 2010 hadi asilimia 43 mwaka jana.

Queen alisema mkoa, pamoja na mikakati mingine, unaendelea kukamata watu wanaowapeleka watoto porini kuwafanyia ukatili.

Awali Mkuu wa Mkoa alisema wamepokea Sh. bilioni 559 za kutekeleza miradi ya maendeleo toka serikalini tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Alisema kwa sekta ya Afya zimejengwa hospitali za wilaya tatu, vituo vya afya 12, kikiwamo cha Wahadzabe katika Kata ya Eshkesh wilayani Mbulu ili kuwasaidia kutibiwa na kuachana na tiba za jadi. Pia alisema zimejengwa zahanati 37 na vimenunuliwa vifaa tiba katika zahanati tisa.

Katika kikao hicho, Msemaji Mkuu wa Serikali, Mubhale Mathinyi, aliwaelekeza wakurugenzi wa halmashauri kuvisaidia vitengo vya mawasiliano ili vitoe taarifa za miradi ya maendeleo.

Vilevile, aliwaagiza wakurugenzi kuwapeleka waandishi wa habari kwenye miradi ya maendeleo ili wananchi wajue matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Manyara, Salimu Bwaya, alisema bajeti imeongezeka zaidi ya mara mbili na barabara za lami zimeongezeka kutoka kilometa 17 mpaka kilometa 30 na madaraja yamefika 405.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Abubakar Kuuli, alisema kwa kipindi cha miaka miwili vimejengwa vituo vya afya vitatu kutoka kituo kimoja kilichokuwapo na zahanati sita zimejengwa.

# Kamati ya Bunge yabaini unyonyaji kwa wakulima

**Na Restuta Damia,** KAGERA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Biashara Viwanda, Kilimo na Mifugo, imebaini kuwapo unyonyaji wa wakulima katika vipimo vinavyosimamiwa na Wakala wa Vipimo nchini (WMA), kwa kufanya ujazo wa lumbesa kinyume cha sheria.

Hayo yalibainika juzi wakati kamati hiyo ilipofanya ukaguzi kwa uwakala huo ambako Mwenyekiti wa kamati hiyo, Deo Mwanyika, alisema kutokana na taasisi hiyo kuwa muhimu kiuchumi, inatakiwa kuhakiki vipimo vinavyotumika katika ununuzi wa mazao ya mkulima kudhibiti unyonyaji.

"Sheria iko wazi na wasimamizi wa sheria wapo, lakini malalamiko bado hayajaisha licha ya kamati kutoa maelekezo ya kuwataka wakala wa vipimo kuhakikisha mlaji, mzalishaji na mkulima wanalindwa kwa kutokuwa na kipimo cha lumbesa yaani kuweka ujazo unaozidi kilo 100," alisema Mwanyika.

Kuhusu kukabiliana na tatizo hilo nchini, Mwanyika alisema kimeundwa kikosi kazi maalum ambacho kinapita nchi nzima na maeneo yanapozalishwa mazao kutafuta chanzo na mwarobaini wa lumbesa kwa mkulima. Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema kutokana na tatizo hilo, wameushauri Wakala huo kuboresha utendaji wake na kujua kero walizonazo wakulima na kuzitatua.

Alisema wafanyabiashara wengi hawako tayari kufuata taratibu za kununua mazao kwa vipimo nao maelekezo ni kuhakikisha wizara kupitia wakala wa vipimo, mazao yote nchini yanauzwa kwa vipimo sahihi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo, Stella Kahwa, alisema kazi yao ni kuhakikisha vipimo vinatumika kwa usahihi, pia kuangalia bidhaa mbalimbali zinavyofungashwa viwandani na mashambani hivyo watahakikisha mtumiaji wa mwisho anapata kilicho sahihi. Alisema suala lumbesa ni mtambuka linalohusisha Wizara mbalimbali hivyo timu maalum iliyoundwa kufuatilia suala hilo ione namna ya kulidhibiti kwa kuwa inamdhulumu mkulima na ikemewe.



Viongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga, wakiwemo maofisa kilimo, ufugaji na umwagiliaji, wakiangalia kilimo cha umwagiliaji cha mboga kwa njia ya matone wanacholima wananchi wa Kijiji cha Dulisi na Wishiteleja, wilayani humo mapema wiki hii, kwa kuwezeshwa na Shirika la Tanganyika Christian Refugee Service(TCRS). **PICHA: MARCO MADUHU**

# Bil. 21/- zapeleka huduma ya majisafi vijijini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MIRADI 14 ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 21.5, imetekelezwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), katika halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga kuanzia Julai 2022 hadi Septemba 2023.

Utekelezaji wa miradi hiyo unaelezwa kusaidia wananchi kuondokana na adha ya upatikanaji wa majisafi na salama na awali walikuwa wakilazimika kutumia maji kwenye mabawa pamoja na mifugo.

Kaimu Meneja wa RUWASA Kahama, Mhandisi Paschal Mnyeti, alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji katika kikao cha wadau wa sekta ya maji kilichofanyika mjini hapa.

Alisema, kati ya 14 iliyoanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2022/2023, miradi 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.7 imekamilika na inaendelea kutoa huduma.

"Miradi hiyo 14 iliyotekelezwa Msalala imepata sita, Ushetu mitano na Manispaa ya Kahama mitatu, hivyo tuwatake wananchi kuendelea kutumia maji hayo ya miradi iliyokamilika na kuacha kutumia yasiyo salama," alisema Mnyeti.

Alisema, mwaka huu wa fedha wamepokea Sh. milioni 322 kwa ajili ya kufanya utafiti wa maji na kuchimba visima virefu katika vijiji 20 vya Halmashauri ya Ushetu vijijini 12 na Msalala vijijini vinane na kwamba watahakikisha wanawahimiza wakandarasi kukamilisha miradi iliyobaki kwa wakati uliopangwa.

Mtaalamu wa Bonde la maji kutoka ofisi ndogo ya Kahama, Elia Samson, aliwataka wananchi kuacha kufanya shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 ya chanzo cha maji hasa kilimo cha umwagiliaji kwa kuwa dawa zinazotumika kwenye mazao zinakuwa na sumu kali na kumwathiri mtumiaji wa mwisho.

Mhasibu wa Chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO) wilayani hapa, Mazolwa James alisema, wanatarajia kusitishia huduma ya maji katika taasisi za umma zinazodaiwa ankara za maji kuanzia Sh. 500,000 na kuendelea kwa kuwa zinasababisha wananchi kukosa huduma kunapotokea hitilafu na kukosa fedha za matengenezo.

James alizitaja taasisi hizo kuwa ni shule za msingi, sekondari, zahanati, vituo vya afya na vituo vya polisi vinavyopatikana Halmashauri za Msalala na Ushetu na kituo cha polisi Ilogi kilichopo kata ya Bulyanhuru kikidaiwa Shilingi milioni moja na kwamba wametoa mwezi mmoja kwa taasisi hizo kumaliza madeni yao.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alizitaka taasisi hizo kulipa ankara za maji wanazodaiwa kwa wakati ili wasisitishiwe huduma kwa kuwa itakuwa aibu shule kuwa na vyoo vya kisasa na kukosa maji hali itakayosababisha watoto kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na uchafu.

# Wanufaika TASAF Bukoba waeleza walivyouaga umaskini

**Na Jenesta Jasso,** BUKOBA

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini mkoani Kagera wameeleza namna mpango huo ulivyowasaidia kujiinua kiuchumi kwa kujenga nyumba bora za kuishi pamoja na uanzishwaji wa miradi ya kiuchumi ukiwemo ufugaji na kilimo chenye tija.

Baadhi ya wanufaika hao kutoka katika Halmashauri ya Bukoba mkoani hapa, wameeleza hayo kwa nyakati tofauti wakiongea na Nipashe kuhusu msaada wa mpango huo kwa kaya maskini na vilevile umewasidia kusomesha wanafunzi hadi ngazi ya chuo kikuu.

Mkazi wa Kijiji cha Rukindo, Kata ya Katoma Gradius Rweyemamu (59), alisema kupitia Mfuko huo alifanikiwa kujenga nyumba bora ya kuishi tofauti na aliyokuwa akiishi hapo awali iliyojengwa kwa nyasi na tope.

Vilevile, alisema amesomesha watoto pamoja na kununua mbuzi kwa ajili ya ufugaji ili kuendeleza mzunguko wa kibiashara na kuacha kuwa tegemezi ili kuendelea kuwahudumia watoto wake wanaendelea na masomo.

Mnufaika Amos Wilfred na mke wake Winfrida Paulo wenye watoto sita wakazi wa Katoma walisema licha ya mradi huo kuwasaidia kujenga nyumba bora, vilevile wameanzisha ufugaji wa nguruwe ambao umebadili maisha yao tofauti na awali.

Mjane na Mkazi wa Bukoba Varelia Sabin (52), mwenye watoto wanne aliishukuru serikali kwa mpango huo kwani familia yake ilikuwa haina uwezo wa kupata mahitaji muhimu lakini sasa kajenga nyumba nzuri, anasomesha watoto pamoja na kumudu mahitaji ya kila siku.

Katika kuendeleza utekelezaji wa mpango huo hivi karibuni, Serikali ya Tanzania ilipokea msaada wa Sh. bilioni 50.13 kwa ajili ya kuufadhili katika kipindi cha pili PSSN II ikiwa Sh. bilioni 45.09 zilitolewa na Serikali ya Uswisi na zaidi ya Shilingi bilioni tano zikitoka Serikali ya Ireland.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, utekelezaji wa PSSN II uliozinduliwa Februari 2020, unagharimu zaidi ya Sh. trilioni 2.2 ukiendana na Dira ya Tanzania ya Mandeleo ya mwaka 2025.

TASAF licha ya kusaidia kaya maskini katika maeneo mbalimbali nchini umesaidia jamii utekelezaji wa miradi ukiwamo ujenzi wa zahanati, madarasa na miundombinu ya maji pamoja na barabara.

Mpaka Desemba 2022 kaya zaidi ya 158,000 nchini zilikuwa tayari katika mpango huo baada ya kutoka katika umasikini uliokithiri na maisha yao kuwa bora.



Ukurasa 14

SIMULIZI ‘WALIVYOULA’ KWA TASAF



**Usakaji pesa unavyowaondoa kinamama Njombe kwenye jukumu kuu kunyonyesha vichanga vyao**

Ukurasa 12

BUFE
IJUMAA NOVEMBA 24, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Mapinduzi kilimo kahawa, Rais alipotanua soko China, nyumbani ofa miche 600,000

- Akubaliana na Rais Mwenza wauzaji kujisajili
- Kigoma, Katavi wachangamkia fursa uzalishaji

**Na Waandishi Wetu**

KAHAWA ni zao kongwe nchini na linashika uchumi wa nchi. Linashika uchumi wa nchi kwa mazao ya Arabica na Robusta, likigusa wilaya kama za Karagwe (Kagera), pia Rungwe na Mbozi (Mbeya), kabla na baada ya uhuru.

Kwa miaka mingi, kuna juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kitaifa, kukuza uzalishaji wake, huku hivi sasa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa katika juhudi kimataifa kukuza soko lake kimataifa, kama ilivyo kwa mazao mbalimbali nchini.

Juhudi hizo za kuinua kahawa sokoni kimataifa, akazifanya Dk. Samia, akiwa ziarani nchini China, mwanzoni mwa mwaka huu.

Kukidhi mkakati unaoendana na makubaliano ya zao la ziara hiyo ya mkuu wa nchi, Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, akawatangazia wafanyabiashara wa kahawa kutoka Tanzania wanaolenga kuuza kahawa katika soko la China, wajisajili kupitia Wizara ya Kilimo nchini.

Balozi Mbelwa akasema, ni hatua iliyolenga kurahisisha usajili wa kampuni za Tanzania zenye nia ya kuuza kahawa China, kwani awali nyingi zilipata changamoto kufanya usajili katika mtandao wa Mamlaka ya Forodha ya China.

Ni zao la ziara hio ya China, Rais Dk Samia akiwa na mwenyeji wake, Rais Xi Jinping wakashuhudia utiaji saini mikataba 15 ya kimkakati, inayolenga kuimarisha ushirikiano, biashara na uwekezaji baina ya nchi hizo mbili.

Januari mwaka huu, kulikuwapo kampuni saba za Kitanzania zilizosajiliwa kuingiza kahawa , hata kutoa uhakika wa soko hilo, huku nchini kukihamasika na kupanua fursa za uzalishaji wake kitaifa.

Wakati Tanzania ikilenga kuongeza uzalishaji wa kahawa kutoka tani 65,235 za mwaka wa kilimo 2021/2022 hadi tani 72,000 mwaka 2022/2023, inalenga kuongeza mauzo yake ya kahawa nchini China.

Inaelezwa, hiyo inafanyika kwa wafanyabiashara wa Tanzania kushiriki Maonyesho ya Uchumi na Biashara ya China na Afrika yaliyofanyika Juni mwaka huu, huko Hunan, China.



Shughuli za ukaguzi wa kahawa wilayani Tanganyika, mkoani Katavi . **PICHA: NEEMA HUSSEIN.**

**KINACHOENDELEA SHAMBANI**

Ikiwa zao la kasi ya uzalishaji na kupanuliwa soko, Taasisi ya Utafiti wa Zao la Kahawa nchini (TACRI), imeanza kujikita kufufua zao hilo kwa kuongeza ushiriki wa wanawake na vijana.

Mtafiti wa Teknolojia na Mafunzo kutoka taasisi hiyo Jeremiah Magese, anasema wanataka kuongeza ushiriki wa wanawake kutoka asilimia 25 hadi asilimia 40.

Ushiriki wa vijana kutoka asilimia 30 hadi asilimia 50, kwa kufanya kuwa wamiliki wa mashamba yao wenyewe.

“Changamoto kubwa iliyopo ni ushiriki wa wanawake na vijana katika kilimo cha kahawa miche iliyopo mashambani imezeeka na waliokuwa wanalima wamezeeka tunaomba wanawake na vijana wajitokeze kulima zao hili kwa kutumia mbegu bora na za kisasa.

“Mpaka sasa kuna jumla ya kaya zaidi ya 300 nchini zinazolima kahawa na kwamba, ili kuongeza wakulima na uzalishaji tunajikita kuzalisha mbegu chotara milioni 20 kwa mwaka, ili baada ya miaka mitano tuweze kufikia miche milioni 100, itakayoongeza uzalishaji hadi kufikia tani laki tatu ifikapo mwaka 2025/2026,”anasema Magese akiwa mkoani Kigoma.

Sofia Malinga, Meneja wa Kanda ya Magharibi, anaiomba serikali kuongeza bajeti ya uzalishaji wa mbegu kutoka laki saba hadi milioni moja na nusu itakayowezesha kuongeza uzalishaji.

Anasema, ongezeko la bajeti litawawezesha pia kutoa elimu kwa maofisa ugani na wakulima wawezeshaji watakaopeleka elimu kwa wakulima ili kuleta ufanisi katika uzalishaji na kufikia lengo la taifa la kuzalisha ambapo mpaka sasa anasema Mkoa wa Kigoma una

Inaendelea Uk 12

FEDHA

# Usakaji pesa unavyowaondoa kinamama Njombe kwenye jukumu kuu kunyonyesha vichanga vyao

- Wanaishia kukiona kipato, 'vichanga' navyo vyapata utapiamlo
- Tabia ya kinababa yatajwa kuchangia sumu hiyo ya makuzi

**Na Elizabeth John, NJOMBE**

SASA imekuwa ukweli kwa wanawake wa Halmashauri ya Mji Njombe, wanakiri kutofuata taratibu za kunyonyesha, kutokana na majukumu mengi ya kiuchumi, hasa kilimo na biashara, mtindo wa maisha nao ukiwa na nafasi yake.

Zao la yote hayo, ni kuwapo uzembe mkubwa katika unyonyeshaji, unaosababisha udumavu wa watoto. Hadi sasa, takwimu za udumavu za taifa, Njombe ikiwa katika mikoa maarufu yenye udumavu wa Watoto inayoongoza kitaifa. Mingine ni Iringa, Ruvuma, Rukwa na Mbeya.

Mkoa wa Iringa unaongoza kwa asilimia 59.9, Njombe asilimia 50.4 na Rukwa asilimia 49.8. Tafiti zilizofanywa na Halmashauri ya Mji wa Njombe, kuangalia hali ya ulishaji watoto chini ya miaka mitano Desemba 2022, unatoa matokeo ya unyonyeshaji sahihi katika kipindi cha miezi sita ya awali, lakini kwenye hatua ya makuzi inabadilika ufanisi unabaki kwa wachache.

Taarifa hiyo inafafanua, wanawake wanaonyonyesha kwa miezi sita ya mwanzo ni asilimia 57; wa miezi 12 hadi 15 ni asilimia 77; huku wanyonyeshaji kati ya miezi 20 hadi 23 ni asilimia nane pekee.

Kunatajwa, utamaduni wa kufanya kazi ngumu mapema kwa siku tatu hadi tano baada ya kujifungua, nayo inatajwa kudhoofisha fursa na uwezo wa wazazi hao wengi kushindwa kunyonyesha kwa muda unaotakiwa kitalaamu; muda mwingine unaopaswa kutumika kunyonyesha, unakuwa kwenye kazi ngumu.

"Nikikaa ndani siku zote hizo nani atanitafutia chakula, mbona nimepona, sina tatizo lolote, nikimaliza kazi atanyonya," ni kauli ya mwanamke aliyetoka kujifungua, akijitetea kwa sababu za kufikia mfumo huo wa maisha.

Ester Mlelwa, mkazi wa mtaa wa SIDO mjini Njombe, anafafanua majukumu ya kiuchumi yanawakwamisha kuhudumia watoto wao, kwa mujibu wa kanuni stahiki.

"Ni vile tunakuwa 'bize' katika kutafuta riziki, kupata chochote kwa ajili ya familia kwa sababu wababa (baadhi yao) ni wavivu kufanya kazi.

"Kufanya majukumu ya nyumbani, wao ni wavivu, wanatuachia sisi wa-mama tusomeshe watoto, tulishe watoto na majukumu mengine hawasimami kama baba, hawasimami kama kichwa cha familia, ili kufanya majukumu yake," anasema.

Ester anapendekeza, ili mama amnyonyeshe mtoto vilivyo, anapaswa kushirikiana na mume, hali inayompa nafasi kumhudumia mtoto kwa usahihi.

Anasema wanaume watakaposimama kwenye majukumu yao, kinamama wanayo nafasi kuzingatia malezi hasa kwenye suala la unyonyeshaji.

"Baba ajirekebishe, asimame kwenye majukumu yake asimuachie mama hasa kipindi akiwa mjamzito na wakati wa kunyonyesha ili mtoto apate afya," anaeleza Ester.



Wanawake wa Halmashauri ya Mji Njombe wakiwa katika Kituo cha Afya Njombe Mjini, wakipatiwa elimu kutoka kwa maofisa lishe wa halmashauri hiyo (hawapo pichani) juu ya kuzingatia siku 1000 za unyonyeshaji. **PICHA ZOTE: ELIZABETH JOHN.**

Flora Kalinga, ana maoni kwamba mzizi wa kinamama wengi kushindwa kunyonyesha kwa wakati, ni kazi nyingi zinazowakabili.

"Kama mimi nimezalishwa tu, nimepanga natakiwa kulipa kodi, ninunue chakula, mpaka saa nyingine unajikuta unasahau kunyonyesha mtoto. Mimi peke yangu ninashindwa," analalamika.

Maria Mwaruka, anayeishi Joshoni, Mjini Njombe, analia na tatizo la hali halisi ya maisha nyumbani kwake, akitamka: "Wakati mwingine unakuta mimi mama nakula chakula ambacho hakikidhi vigezo, mtoto inabidi anyonye sasa nitafanyafanyaje?"

"Ndani hakuna chakula, mimi mama inabidi nile chakula kinachojitosheleza ili mtoto anyonye, inanipasa niende nikatafute kusudi mtoto aweze kunyonya."

Hata hivyo, Maria anakiri kufahamu msisitizo wa wataalamu afya kuhusu umuhimu wa watoto wachanga kupata maziwa ya mama, baada ya kuzaliwa, kwani inajulikana maziwa ya mama humpatia mtoto virutubisho anavyohitaji miezi sita ya mwanzo tangu kuzaliwa.

**JICHO LA KINABABA**

Baadhi ya wanaume, akiwamo Amiri Galus, mkazi wa Njombe, anakiri kuwa ni kweli wanawake wameachiwa majukumu ya kulea familia, akitaja sababu ni wanawake wenyewe kujikita kwenye utafutaji riziki.

"Unakuta mwanamke yupo 'bize'sana kwenye majukumu, muda anaporudi kwenda kumnyonyesha mtoto unakuta hatamani tena, kwa sababu anakuwa ameshapitiliza muda wa kunyonya.

"Pia wanawake wa namna hiyo sasa wanaingia kwenye majukumu ya kuanza kumlisha mtoto chakula, wakati ni mdogo labda ugali, uji wakati anatakiwa kupata maziwa.

"Shughuli nyingi ndizo zinazosababisha kucheleweshwa watoto kupata maziwa ya mama na hii inafanyika kwa sababu kwa kiasi kikubwa watu wote tunapambana, mwanamke anapambana na mwanaume anapambana," anasema Galus.

Basilius Mligo mkazi wa Njombe anaungana na hoja hiyo ya wanaume, kwamba wanawake wana majukumu makubwa, hususani kwenye ujasiriamali.

"Unaweza ukakuta asubuhi wameamkia kwenye tenda wanafanya kazi mpaka labda saa saba mchana, wanarudi nyumbani saa nane, kwa hiyo ni kweli wanaweza wakashindwa kutekeleza majukumu ya kuwatunza watoto," anasema Mligo, akishauri kuendelea kutolewa elimu kwa kinababa wasiwape majukumu makubwa kinamama.

"Baba ndiyo wa kwanza katika nyumba, ni kichwa cha nyumba. Inatakiwa yeye ashughulike zaidi kuliko mama ili aitunze familia ikae vizuri, lakini kama baba anakuwa yeye ni mzururaji, mama ndiye anayefanya kazi kubwa ndiyo inaathiri masuala ya unyonyeshaji," anasema Mligo.

**SURA YA UTAFITI**

Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania TDHS, idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee imeongezeka kutoka asilimia 59 ya mwaka 2015/2016 hadi asilimia 64 mwaka jana.

Takwimu pia zinaonyesha watoto wanaonyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, zimeongezeka kutoka asilimia 53.5 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 70 mwaka 2022.

Shirika la Afya Duniani (WHO), limeweka malengo ya kunyonyesha watoto bila ya kuwapa kitu kingine chochote kwa miezi sita, wafikie asilimia 50 ifikapo mwaka 2025.

**OFISA LISHE.**

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Michael Swai, anaungana na wanaokiri kuwapo changamoto ya unyonyeshaji, akinena: "Ni wanawake kushiriki zaidi katika shughuli za kiuchumi badala ya malezi.

"Tunawaita wanaume wengi na kukaa nao tunawaeleza na wanapokea, tunawapa elimu, tunajaribu kuwaambia wawapunguzie majukumu wanawake kipindi wanakaribia kujifungua na baada ya kujifungua, ili kusaidia watoto kunyonya kwa wakati ili kupata maziwa bora.

"Kuna tabia mwanamke baada ya kujifungua anakaa labda wiki mbili tu anaambiwa aende shambani. Tunawaambia jamani!...Hata serikali imetoa 'maternity leave' (likizo ya uzazi) kwa wafanyakazi wake kwamba mama akijifungua anapewa siku 84 kwenda juu. Kwa hiyo na nyie tunaomba wanawake zenu kabla kujifungua na baada ya kujifungua muwape muda wa mapumziko."

Swai anaendelea: "Unakuta shambani anaenda na mtoto na anamnyonyesha pale mtoto anapolia. Vile vile hata maziwa ya mama yanakuwa hayana ubora, kwa sababu anakuwa anahangaika jua, baridi kwa hiyo hayo yote tumewaelimisha wanaume wawape mapumziko."

Swai anataja changamoto nyingine ni kuwapo kwa ndoa za mitala, akiwa na ufafanuzi: "unakuta mwanaume ana nyumba tatu au nne, kila mtu yupo kwake. Ameacha mzazi nyumbani, lakini hajui atakula nini mchana, amekula nini jioni wao ukiwatafuta hawaonekani na wapo 'bize'," anasema Swai.

**RC NJOMBE**

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, mara nyingi amekuwa akikemea udhaifu huo katika jamii yake, kinamama wa mkoa wake si wa kuthamini unyonyeshaji watoto wao.

"Mkoa wa Njombe wanaoongoza kwa kumiliki uchumi ni kinamama na akishajifungua anapika makande anaacha ndani wiki nzima mtoto anakula makande kuanzia asubuhi mpaka asubuhi, wiki nzima yeye yupo kwenye kutafuta, matokeo yake watoto wanapata shida ya afya," anasema Mtaka.

Mtaka anataja hatua za kukabili, wanashirikiana na taasisi za kinamama na kidini, kuhakikisha wanatoa elimu kwa wanawake kutambua umuhimu wa kunyonyesha watoto kwa siku 1,000 za mwanzo wa uhai wake.

Ni hivi karibuni, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa ziarani Njombe, naye akasisitiza suala la unyonyeshaji, akiwataka wanawake mkoani humo kuhakikisha wanazingatia siku 1,000 za unyoyeshaji.

"Akishajifungua, hakikisheni mama anakula vizuri chakula chenye virutubisho... Kwingine wanajua kabisa, ili tuendelee kuzaa watoto wenye uwezo mkubwa wa kufanya biashara wa kuwa viongozi, bongo zinawaka shuleni, ni lazima wawe wananyonya vizuri kwa kipindi hicho cha miaka walau miwili.

"Mama zangu msitake urembo kwa kuacha kunyonyesha, muache hizo furaha za wazee 'akina sisi', nyonyesheni watoto vizuri nayasema haya kwa sababu ni jambo kubwa," anasema Dk. Mpango.

# MAPINDUZI KILIMO KAHAWA, RAIS ALIPOTANUA SOKO CHINA, NYUMBANI OFA MICHE 600,000

Inatoka Uk 11

wakulima wawezeshaji 15.

Vilevile, Bodi ya Kahawa Tanzania iligawa miche ya kahawa katika kijiji cha Mwese, kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, ambako kazi hiyo iliongozwa na Mkuu wa Wilaya, Onesmo Buswelu.

Buswelu anasema miche hiyo wameigawa bure kutokana na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kulipia takribani Miche 600,000.

"Iwapo miche hii yote itatunzwa na ikafanikiwa kustawi itatupatia matokeo makubwa kutoka kwenye kuzalisha tani 5,000 msimu uliopita kwenda kwenye tani 100,000 ifikapo mwaka 2028.

"Sasa hii maana yake nikwamba wote mliopata miche leo na watakaopata miche kesho na kuendelea, kwa sababu zoezi hili lipo mpaka mwezi wa nne, inategemea na mvua.

"Tunawaomba sana na kuwasihi sana, hii miche isiende kutelekezwa. Miche hii ni yetu Watanzania, ni uchumi wetu na uchumi wetu ndio ustawi wa taifa letu.

"Tunafahamu kwamba kahawa inauzwa katika soko la ndani na la nje (ikiwamo China), lakini asilimia kubwa ni soko la nje. Sasa maana yake ni nini? Tutakapokua tumezalisha kwa wingi kipato kikubwa kitaongezeka kwenye mifuko yetu.

"Wito wangu kwenu nyote, tuanze na maofisa ugani, Ofisa Kilimo wa Wilaya, maofisa mazao na wataalamu wote wanaohusika na kilimo wahakikishe kwamba kuanzia leo wanafuatilia miche yote, kuanzia tuliyogawa hapa inafika na kupandwa kwenye mashimo ambayo yameandaliwa na inatunzwa na kuhifadhiwa.

"Wakulima mlioko hapa, tunaomba sana muwe wasikivu na muwe wafuatiliaji, mpokee maelekezo na ushauri wa wataalamu wetu ili kupata tija na ufanisi katika zao hili la kahawa, ambalo pesa yake iko 'njenje'..."anasema Mkuu wa Wilaya Buswelu.

Taarifa iliyosomwa kwa mkuu wa wilaya, inafafanua changamoto za kilimo cha kahawa, ikijumuisha kuhusika na wazee peke yake na vijana wakikimbia kilimo hicho, wakidai fedha zake hupatikana baada ya muda mrefu.

Aidha, kuna madai ya soko lake sio la uhakika hali, inayosababisha wakulima kuuza kahawa yao kwa walanguzi na changamoto ya mwisho ni bei kubwa ya pembejeo za kilimo.

Ofisa Maendeleo zao la Kahawa, Kanda ya Magharibi Jasson Michael, anasema Bodi ya Kahawa Tanzania imeweka mpango wa kuongeza uzalishaji kutoka tani 82,000 kitaifa hadi kufikia tani 300,000 kitaifa.

Anasema kwa kijiji cha Mwese au Tanganyika kwa ujumla uzalishaji, umekuwa kidogo na wameanza kulima tangu mwaka 1980, hawajawahi kuvuka tani 10 kwa mwaka, akisema mpango mkakati wa bodi ni kutoka tani hizo 10 hadi tani 100 ndani ya miaka nane ijayo.

**SAUTI YA WAKULIMA**

"Hili zao nimelilima tangu mwaka 1984, baada ya kutoka vita ya Iddi Amini, nilikuta baba angu analilima sana na mimi nikaanza, nina vijana wangu wote wamekimbilia mjini na majumba yao, kwa hiyo hili zao kwa Mwese limebaki ni la wazee tu sikufichi!

"Hiki kilimo kimenisaidia nimesomesha nimejenga hata ukija kwangu kuna TV natizama taarifa ya habari ndani kwa ndani wala sitoki nje sijui kwenye vigenge, hapana!

"Naomba viongozi wa vijiji, kuna vijana huwa wanaenda kwenye 'Puli' basi wajaribu kuwadhibiti hawa vijana, ili waweze kuzingatia hiki kilimo,"anasema Invocavit Shoo, mkulima wa kahawa.

"Zao la kahawa nimetokea kulipenda zamani kipindi nakua ndio nilikua naona wazazi wangu wanalima Kahawa kwa baadae nilivyoanza kujitegemea na kuona kuna mtu aliuza pesa nyingi sana, nikaanza na mimi kununua miche ya kahawa kipindi hicho tulikuwa tunanunua shilingi 50.

"Nikanunua, nikapanda baada ya mavuno, nikaanza kupata hela ya matumizi, baadae nikaanza kukua ila hela yake inahitaji uvumilivu maana huwa tunavuna mwezi wa sita na kupata pesa ni mwezi wa 10. Kwa hiyo, muda huo ndio unatakiwa uandae shamba na watoto ndio wanataka kutoka shule warudi kwahiyo unakuta ile hela inanisaidia," anasema Venera Kanizius, mkulima wa kahawa.

- **Adela Madyane-Kigoma na Neema Hussein, Tanganyika**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Wenye mtazamo kama George Weah kwenye jamii zetu wako wangapi?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

KWA kweli Waafrika tunatofautiana sana katika masuala ya fikra, hisia, hulka na mitazamo, hususan linapokuja suala la maslahi ya kimaisha na kisiasa, hapo ndipo mtu hutamani kuua mwenziwe ili apate akitakacho.

Ukifuatilia kilichojiri katika taifa la Liberia hivi karibuni, utaelewa ninamaanisha nini, hasa unapolinganisha na mapigano na vita vya wenyewe vinavyotokea na kuendelea katika baadhi ya mataifa.

Utaelewa ni kwanini, baadhi ya mataifa hayo yamepitia mapinduzi kwa kuondoa serikali halali zilizochaguliwa na wananchi na hiyo ikisababishwa na kutoridhika, pia kutopenda kuachia madaraka kwa wakati mwafaka.

Hivi karibuni, wananchi wa Liberia waliamua kumchagua Mzee Joseph Boakai kuwa Rais wao, katika uchaguzi mkuu, akimshinda aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, George Weah ambaye naye alichaguliwa na wananchi wa taifa hilo kwa mihula miwili tofauti.

Katika uchaguzi huo mkuu unaofanyika kila baada ya miaka mitano kama tufanyavyo Tanzania, Boakai alimshinda Weah kwa tofauti ya kura 28,000 pekee na Rais huyo aliyepita, kukubali kushindwa bila ya kulalamika.

Rais Mteule Boakai mwenye umri wa miaka 78, alipata asilimia 50.58 ya wapiga kura 1,431,388 waliojitokeza kuchagua, huku mchezaji maarufu na nguli wa soka duniani wa zamani Weah, akipata asilimia 49.42.

Hata hivyo, ushindi wa Boakai ulikuja baada ya uchaguzi kurudiwa, kutokana na awamu ya kwanza iliyopigwa Oktoba 10 mwaka huu, mshindi kupata kura chini ya asilimia 50, tofauti na matakwa ya katiba

yanayotaka mshindi apate zaidi ya asilimia 50.

Boakai alipata asilimia 51 dhidi ya asilimia 49 za Weah, kwenye duru la pili la uchaguzi huo na ilipotangazwa, mshindwa, alimpigia simu mshindi kumpongeza, huku akisema aliyeshinda si Boakai bali ni Liberia na kutaka maslahi ya taifa yapewe kipaumbele.

Weah alikubali kwa roho nyeupe ushindi wa Boakai na kumpongeza kwa ushindi huo, huku akiwataka wafuasi wake wakubaliane na matokeo hayo, kwa maslahi mapana ya taifa lao.

Ni dhahiri kuwa, kiongozi huyo wa zamani wa Liberia, ameonyesha mfano mzuri wa kukubali matokeo na kuwasihi wafuasi wake kutulia, ili kuepusha vurugu ambazo zingeweza kutokea kama asingekubali kushindwa.

Na hiyo inazingatia hali halisi ilivyo katika mataifa mengi ya Afrika Magharibi, kunakotokea mapinduzi ya hapa na pale, hivyo endapo angesema amedhulumiwa, ni dhahiri watu wangeingia mitaani kupinga dhuluma na matokeo yake kuwa vurugu.

Hivi kwa hapa Bongo mathalan itokee hivyo, kwamba mpinzani kashinda kwa asilimia 51 na aliyekuwa madarakani kaanguka kwa kupata asilimia

49, nini kitatokea? Tujiulize tu katika mazingira ya siasa za kwetu hapa Tanzania.

Niseme, Weah anapaswa kuchukuliwa na viongozi wa kisiasa wa Afrika, kama mfano wa kiongozi asiye na uchu wa madaraka, kwa sababu kwa umri wake wa miaka 57, asingetaka kuachia madaraka hayo kirahisi kwa mzee wa miaka 78.

Boakai ni Rais wa 26 wa Liberia tangu mwaka 1848 baada ya taifa hilo lilipopata uhuru wake mwaka 1847, ambao katikati lilipitia misukosuko mingi hadi ilipopata rais mwanamke mwaka 2006, Ellen Johnson Sirleaf.

Rais Ellen alileta utulivu nchini humo, kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan anavyofanya kurejesha utulivu na kuponya majeraha katika nafsi za baadhi ya Watanzania na kuliweka Taifa sawa.

Weah anakuwa kiongozi wa mfano Afrika anayeamini katika demokrasia, kwa kukubaliana na hali halisi ya kisiasa nchini mwake na hivyo kutakiwa kuigwa na wanasiasa wengine duniani, wakiwamo wa Kitanzania.

Tunakwenda kwenye uchaguzi mwakani na mwaka 2025, ni nini tunajifunza kutokana na uchaguzi wa Liberia? Kati yetu wapo wanaodhani kwamba, kila anayechaguliwa kuongoza nchi basi nafasi hiyo inakuwa kama hatimiliki yake.

Kwamba akishakalia kiti, basi hakuna wa kumtoa. Kwa Weah tujiulize, nini kilimfanya awe 'Rahim' kiasi kile hata kukubali matokeo ya kauli ya Waliberia na kuahidi kushirikiana na Rais mpya, kuijenga nchi hiyo. Je ni ukwasi alionao na kutoendekeza umasikini?

Au, mchezo wa soka ulimjenga kuwa na roho ya upendo kwa wenzake na taifa? Hakika watu aina ya George Weah ni wachache Afrika na huenda ikawa hata kwa wanasiasa wa Bongo, dhana na unasaba wa matumbo binafsi.

Hakika bado tuna safari tuendako! Mungu tubariki!

UCHUMI

# SIMULIZI 'WALIVYOULA' KWA TASAF

- Amenufaika 'hadi basi', aomba kujitoa
- Mlo safi, mahudhurio kliniki yavutia
- Vizazi sasa vina wasomi vyuo vikuu
- Nyumba, mifugo, shamba kila familia

**Na Shaban Njia, SHINYANGA**

WANUFAIKA wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) mikoa ya kanda ya Ziwa na Magharibi, wameeleza namna mfuko huo ulivyowasaidia katika kuwainua kimaisha ikiwamo kusomesha watoto wao mpaka elimu ya juu kwa kupanga matumizi sahihi kulingana na ruzuku wanayopata.

Aidha, wanufaika hao ni waliosajiliwa kwa mara ya kwanza na kupokea ruzuku zao tangu mwaka 2015.

Kiwango cha chini cha ruzuku wanazopokea kila baada ya miezi miwili ni Sh.20,000 na kuna baadhi wanapokea mpaka kiasi cha Sh.100,000 kwa sababu ya kuwa na watoto wanaosoma, wapo wenye umri chini ya miaka 18. Pia kuna mahudhurio mema ya kliniki kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Utoaji ruzuku hizo kila baada ya miezi miwili, huendana sambamba na zoezi la utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa walengwa, kilimo chenye tija na ufugaji wa mifugo hali ambayo wengi wameitikia kuondokana na umaskini.

Katika mikoa ya kanda ya Ziwa na Magharibi ni miongoni mwa mikoa yenye walengwa walionufaika na TASAF kwa kuzielekeza ruzuku katika kilimo na kusomesha watoto wao mpaka elimu ya juu.

Miongoni mwa miradi ya maendeleo ambayo ilitokana na mfuko huo kwa walengwa ni pamoja na ile ya kilimo, ufugaji kuku, bata na wanyama, ambayo kwa sasa kila familia ilipata ruzuku na kujikwamua kiuchumi.



Mariam Rashidi (47) mkazi wa Kijiji cha Molemlimani kata ya Mole Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora, akiwapatia chakula mbuzi wake 20 aliowapata baada ya kupokea ruzuku ya TASAF tangu mwaka 2015 mpaka sasa. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

### WALENGWA WANAVYONENA

Hawa Omary (60) mkazi wa kijiji cha Ishinabulandi kata ya Samuye Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, amefanikiwa kujenga nyumba ya kisasa na kufuga kwa kisasa baada ya kupokea ruzuku ya TASAF kwa mara ya kwanza kiasi cha Sh.44,000 mwaka 2015.

Anasema, kulingana na umri wake kuwa mkubwa fedha aliyokuwa akiipata alihakikisha anaelekeza kwenye shughuli zenye tija ikiwamo ufugaji kuku, bata, mbuzi, chakula cha familia na kiasi kingine ananunua vifaa vya ujenzi.

Omary anasema, wingi wa mbuzi alionao na namna anavyoshirikiana na wajukuu zake katika kuwafuga na malisho kwa mbuzi mmoja ana uwezo wa kuuza kwa gharama ya Sh.60,000 hadi 80,000 kulingana na ukubwa wake na sasa hana shida ya ukosefu wa chakula ndani kama ilivyokuwa hapo awali.

Magdalena Ibrahim (60) wa kijiji cha Ipoja kata ya Sigili Halmashauri ya Nzega mkoani Tabora anasema, kilimo chenye tija na kufuata maelekezo ya watalaamu wa kilimo waliopo kila kata kimewezesha kunufaika na TASAF kuzalisha zao la mpunga kwa tija na kujenga nyumba ya kisasa na yenye hadhi kijijini.

Ibrahimu anasema, kiasi hicho aliamua kukodisha shamba la ekari moja kwa Sh.100,000 na kulima mpunga kitaalamu na kufanikiwa kupata magauni nane ambayo yote aliyauza na kupata Sh.720,000 na ilikuwa mwaka 2016 na kuanzisha ujenzi wa msingi wa nyumba yake.

Anaendelea kusimulia, mwaka 2017 alipata nguvu na kukodisha shamba ekari tatu kila moja Sh.100,000 sawa na Sh.300,000 na kupata magunia 22 ya mpunga na aliyauza yote na kupata Sh. milioni 2.2 kwa wastani wa Sh.100,000 kila moja na kuanza kupandisha ukuta wa ujenzi na fundi alikuwa mtoto wake na sasa anaishi kwenye nyumba yake ya kisasa.

### TASAF WANAFUNZI

Mkazi wa Mtaa wa Shunu, Salumu Hamisi (21) ni mwanachuo aliyenufaika na ruzuku ya TASAF kwa kusomeshwa na wazazi wake baada ya kupokea ruzuku hiyo tangu akiwa shule ya msingi, sasa yupo Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania, jijini Mwanza na kupata mkopo wa elimu kwa asilimia 100.

Anasema, yuko mwaka wa pili sasa anasoma shahada ya Elimu ya Jamii na amechukua fani hiyo kutokana na watu wengi kuwa na matatizo, kipindi cha likizo huwa anaenda kujifunza ufundi wa magari na wakati mwingine anafanya kazi ya kujitolewa katika ofisi za TASAF, Manispaa ya Kahama kama sehemu ya kupata uzoefu kazini.

Grace Mahona (23) anaeleza kuwa mfuko huo umemsaidia katika masomo yake kuanzia shule ya msingi hadi sasa yuko Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam (UDSM) mwaka wa pili, shahada ya ualimu.

Mwenzake, Elizabeth Bundala (18) anasoma kidato cha pili, anafurahishwa na wazazi wake wanapopokea ruzuku humshirikisha kupanga matumizi na yeye anapata nafasi ya kueleza mahitaji yake.

Anasema, wazazi wake walipata shamba kubwa la ekari saba, kati ya hizo tatu zinatumika kulima mpunga, bustani na mazao mengine na ekari nne wanalima mahindi.

### AOMBA KUTOLEWA TASAF

Mrisho Bundala (46) wa Kijiji cha Wame Kata ya Kilago Manispaa ya Kahama, anaomba kutolewa kwenye upokeaji wa ruzuku ya TASAF baada ya kufanikiwa kumiliki makazi ya kisasa, mifugo na kuwa na mashamba ya kumpatia chakula cha kutosha msimu mzima kila mwaka.



Mkazi wa kijiji cha Ipoja kata ya Sigili Halmashauri ya Nzega mkoani Tabora Magidalena Ibrahim (60) akiwa amesimama mbele ya nyumba yake aliyojenga kutokana na ruzuku ya TASAF anayopokea kila baada ya miezi miwili.

Anasema, alisajiliwa na kupokea ruzuku yake kwa mara ya kwanza mwaka 2015 akianza na Sh. 48,000 na kushirikisha familia yake hususani mkewe Maria Charles (37) na binti yake wa kwanza, wakakubaliana kununua mbuzi na kuanza ufugaji na kiasi kingine wakanunua chakula cha familia.

Bundala anasema, mara ya mwisho kupokea ruzuku yake ilikuwa mwezi Novemba na Desemba mwaka 2022, alifika katika Ofisa za TASAF Wilaya ya Kahama na kuomba kuondolewa kwenye mpango, ili wengine wapewe fursa hiyo, yeye ana uhakika wa kupata chakula tofauti na awali.

"Mkutano wa hadhara kijiji ulipendekeza jina langu kwa watu wa TASAF kuwa mie maskini, na nikweli kwa sababu kula yangu ilikuwa ya shida na niliogopa mpaka kuzaa kwa sababu sikujua wakija Duniani watakula nini ila sasa ninanyumba, mashamba ekari saba, ng'ombe wa kilimo, mbuzi 15 na chakula ndani ya kutosha," anasema Bundala.

### UFUGAJI WENYE TIJA

Mariam Rashidi (47), mkazi wa Kijiji cha Molemlimani kata ya Mole Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora, anasema, ushirikishaji wa familia katika kupanga matumizi ya fedha zinazotolewa na TASAF umemuinua katika ufugaji wa mbuzi na kuezeka nyumba yake kwa bata.

Anasema, kulingana na umri wake kuwa mkubwa alijikita kwenye ufugaji wa mbuzi na kuanza na mbuzi wawili ambao walizaliana kwa wingi na sasa ana mbuzi 20 kila anapopata shida anauza kadhaa kukidhi shida zake.

Haraja Mhoja (45) mkazi wa kijiji cha Mkolye Halmshauri ya Sikonge, anasema kulima mazao ya chakula, biashara na mikunde kwa kufuata ushauri wa Ofisa Kilimo kumesababisha kupata mavuno mengi na kuanzisha ufugaji wenye tija wa ng'ombe.

Anasema, kila anapopokea ruzuku yake Sh.52,000 akazielekeza kwenye kununua pembejeo za kilimo na akihakikisha anamshirikisha Ofisa Kilimo wa Kata. Msimu wa kwanza alipata gunia 16 na kuziuza zote na kupata Sh. milioni 1.3 fedha ambazo hakutarajia kuzipata kutokana na umri aliokuwa nao.

Mhoja anasema,baada ya mauzo alilazimika kununua ng'ombe wawili kwa Sh.1,200,000 kwa wastani wa Sh.600,000 kila mmoja na fedha iliyosalia alinunua chakula cha familia ikiwamo mahitaji ya watoto wake shule kwani ana familia ya watu 12, na sasa ana ng'ombe 13 wa maziwa.



# Uhaba wataalam vifaa tiba pigo nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imesema soko la ajira nchini linahitaji wataalam wa vifaa tiba na kukosekana kwa watalaam hao nchini ni pigo kubwa.

Akifungua Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Umoja wa Wahandisi wa Vifaa Tiba (AMETT) jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Mafunzo na Rasilimali Watu wa wizara hiyo, Dk. Saitore Laizer, alisema soko la ajira la watalaam hao ni kubwa na kuomba vyuo vitoe mafunzo yatakayozalisha watalaam wa kada hiyo.

"Tasnia zinazokua kwa kasi ni teknolojia ya vifaa tiba na kwa sasa vifaa vingi ni vya kidijitali. Inahitajika kuendelea kujiendeleza kielimu ili kutozungumzia teknolojia iliyopitwa na wakati.

"Niombe vyuo vizingatie hili, pia wafundishe kinachoendana na yanayoendelea duniani," alisema kiongozi huyo.

Dk. Laizer alisema wizara iko tayari kuwaendeleza watalaam hao ndani na nje ya nchi na kuwahimiza watalaam kujiendeleza na serikali itaendelea kutafuta fedha za kuendeleza taaluma hiyo.

"Kwa Mwaka 2019 Sh. bilioni 1.84 zilitengwa kwa ajili ya kuendeleza watalaam na mwaka 2020 ilipanda ikawa Sh. bilioni 3.6 na mwaka uliofuata bajeti ilipanda hadi Sh. bilioni tano na mwaka uliofuata bajeti ilipanda hadi Sh. bilioni nane na mwaka huu wa fedha katika mfuko mkuu wa serikali peke yake kuna bajeti ya Sh. bilioni tisa," alisema.

Dk. Laizer alisema serikali imewekeza katika kununua na kusimika vifaa tiba, lakini bado watalaamu wanaozalishwa hawakidhi mahitaji yaliyopo.

Vilevile, alisema watumishi wa vifaa tiba 280 wameajiriwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2023.

Aliahidi serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya umoja huo.

Awali Rais wa umoja huo, Valentino Vanga aliomba serikali iajiri wahandisi na mafundi sanifu wa vifaa tiba ili kufikia kama inayopendekezwa.

"Kuna upungufu wa watalaam hawa, kuna hospitali zina mtaalam mmoja hasa ikizingatiwa serikali imewekeza kwa sasa vifaa vingi kwenye hospitali zetu," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na serikali kuimarisha sekta ya afya, watahakikisha vifaa tiba vilivyonunuliwa vinatunzwa na kufanyiwa matengenezo mara kwa mara.

Aliomba serikali kuanzisha Baraza la Kitaaluma la Wahandisi hao ili kuongeza chachu kwa umoja huo.



Kamishna Msaidizi wa Idara ya usimamizi wa madeni wa Wizara ya Fedha, Omari Khama (kushoto) na Kamishna idara ya usimamizi madeni wizara hiyo, Japhet Justine (wapili kushoto), wakijadiliana jambo na VIsions Tigkarakis kutoka Uingereza na Rafael Molina kutoka shirika la Global Fund, walipokutana kwenye semina, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Muhimbili yaanza kutoa matibabu kwa mtandao

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia (DIT) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) wameanza kutoa matibabu kwa njia ya mtandao nchini. Mkurungenzi Mkuu wa mfuko huo, Justina Mashiba alibainisha hayo juzi alipotoa taarifa yake kwa wajumbe wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar walipotembelea mfuko huo jijini hapa.

Mashiba alisema mfuko huo kwa kushirikiana na taasisi hizo wameanza kutoa matibabu kwa njia ya tiba mtandao ambayo mgonjwa anatibiwa nje ya nje ya Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Alizitaja hospitali zingine zilizounganishwa kwenye mtandao huo kuwa ni pamoja na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro na zinazokamilishwa ni pamoja na Ruvuma, Tanga, Katavi, Nzega na Chato.

Alibainisha kuwa kwa upande wa Zanzibar, hospitali zilizounganishwa kwenye mtandao tiba ni Hospitali ya Abdala Mzee iliyoko Pemba na Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja iliyoko Unguja ambako utekelezaji wake uko katika hatua za mwisho.

Alibainisha kuwa lengo la mfuko huo ni kuhakikisha wanaunganisha hospitali zote nchini kwenye mtandao huo ili wananchi wapate unafuu wa gharama za kufuata matibabu mbali.

Pia alisema UCSAF imepanga kutoa vifaa 250 vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma hiyo na zaidi ya wasichana 954 wamepata mafunzo hayo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016. Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, wasichana 110 watapatiwa mafunzo katika mikoa ya Songwe (30), Tabora (40) na Kigoma (40) na katika mradi huo, UNICEF imechangia kwenye bajeti yao.

"Kwa Zanzibar vituo 11 vimejengwa ambapo Pemba ni vituo vinne na upande wa Unguja ni vituo saba. Kituo cha mwisho ni kilichojengwa Bwefum, kilizinduliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. Kilijengwa kwa gharama ya Sh. milioni 147," alisema.

Alivitaja vituo vingine kwa Zanzibar kuwa ni pamoja na Tunguu, Mwera, Kitogani, Mkokotoni, Kiembe Samaki, Mahonda, Wete, Machomanne, Micheweni na Jonza.

Pia alisema minara 758 itajengwa katika kata 713 kwenye mikoa 26, wananchi milioni 8.5 watanufaika na mradi huo ambapo kampuni ya Airtel itajenga minara 169, TTCL minara 104, Honora (Tigo) minara 261, Halotel minara 34 na Vodacom minara 190. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Yahaya Rashidi Abdalah alishukuru kwa miradi inayotekelezwa kwenye maeneo mbalimbali na wameona jinsi ambavyo wananchi wananufaika na huduma za mawasiliano.

# Shirika lakabidhi miradi yake kwa serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Sustainable Environment Management Action (SEMA) limekabidhi kwa uongozi wa Mkoa wa Singida miradi sita ambayo limetekeleza kwenye Halmashauri za Wilaya ya Iramba, Ikungi na Manyoni, ikigharimu zaidi ya Sh. bilioni 4.5.

Miradi hiyo ilikuwa inatekelezwa na shirika hilo kuanzia mwaka 2019 hadi mwaka huu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwamo Shirika la Strommer Foundation East Africa.

Mkurugenzi Mkuu wa SEMA, Ivo Manyaku akizungumza juzi katika kikao cha kukabidhi miradi hiyo kwa Serikali, aliitaja miradi iliyotekelezwa katika kipindi hicho ni pamoja na uwezeshaji jamii kiuchumi na mradi wa kuweka akiba na kukopa wa WEKEZA.

Mingine ni mradi wa Bonga (NJOO TUONGEE), mradi wa elimu ya mafunzo ya ufundi kwa vijana (TUNAWEZA), mradi wa elimu ya awali na makuzi, mradi wa kuzijengea uwezo asasi za kiraia na mradi wa uwezeshaji jamii kilimo biashara.

Alisema miradi hiyo imewanufaisha watu takribani 450,000. Ililenga kukabiliana na umaskini kwenye makundi ya jamii - vijana, wasichana na watu wenye mahitaji maalum.

Manyaku alitaja malengo mengine ya miradi hiyo ni kuboresha uchumi kwa walengwa, afya na lishe, elimu jumuishi, huduma ya maji na usafi wa mazingira, utawala bora, kilimo na mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Katibu Tawala Msaidizi, Utawala na Rasilimali Watu, Stephen, Pancras aliwataka maofisa maendeleo ya jamii wa halmashauri za wilaya mkoani Singida kuhakikisha wanawahamasisha wananchi kujiunga kwenye vikundi ili idadi ya wanufaika wa miradi hiyo iwe kubwa.

Pancras pia alipongeza juhudi za wadau mbalimbali wa maendeleo mkoani Singida wakiwamo SEMA na Strommer Foundation East Africa ambao kwa kiwango kikubwa wameleta tija na ustawi wa maisha kwa wanaSingida.

Ofisa Elimu Mkoa wa Singida, Dk. Elpidius Baganda alipongeza shirika hilo (SEMA) kwa kutekeleza miradi ya sekta ya elimu na kuwa elimu ikitolewa kwa wananchi, ndio suluhisho la mambo mengi katika maisha ya wanadamu.Baganda alitumia nafasi hiyo kuipongeza serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ambayo yanayafanya mashirika hayo yasiyokuwa ya kiserikali kutekeleza miradi yao pasi na bughudha zozote.

Shirika la SEMA lilisajiliwa nchini Machi 10,1998 na kuanza rasmi shughuli za utekelezaji Januari Mosi, 2000 na lilipata hati ya ukubalifu (Certificate of Compliance) Machi 9, 2006 na makao yake makuu yapo Manispaa ya Singida eneo la Utemini (Mtaa wa Viwanda).








Malori mawili yakiwa yamegongana na kufunga barabara kuu ya Mbeya – Njombe, eneo la Mabadaga, wilayani Mbarali mkoani Mbeya juzi, kitendo kilichosababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachimbaji wadogo walia wawekezaji kupoka migodi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu katika Kijiji cha Mwaoga, Kata ya Makongolosi, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya wameiomba serikali kuingilia kati kuwaondoa baadhi ya wawekezaji ambao wanavamia maeneo yao.

Wanadai baadhi ya wawekezaji hao ambao wamepatiwa leseni na serikali za kuchimba madini, wamekuwa wanapanua mipaka yao na kuingia kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo na kuanza kufukia mashimo yao.

Ni malalamiko yaliyotolewa juzi na wachimbaji hao walipozungumza na wandishi wa habari, wakidai wamekuwa wanashindwa kufanya shughuli zao kwa amani kutokana na kuwaogopa wawekezaji hao.

Mmoja wa wachimbaji hao, Furaha Nyembela alisema yeye pamoja na wenzake walianzisha mgodi katika eneo hilo, lakini mmoja wa wawekezaji akajitokeza na kufukia mashimo yao akiwataka kuondoka kwa madai kuwa eneo hilo ni lake.

Alidai waliamua kwenda kwa Mkuu wa Wilaya kuomba msaada, lakini wakajibiwa kwamba wanatakiwa wasiendeleze shughuli zao kwenye eneo hilo kwa sababu ni la mwekezaji ambaye ameshafanyia utafiti.

Alisema waliambiwa wahamie kwenye eneo lingine ambalo wao wanaamini halina dhahabu kama ilivyo kwenye eneo hilo la awali.

"Sisi tumeshachoka, tumekimbia vya kutosha na mwekezaji huyu ameamua kutufuata mpaka chumbani, kitakachofuata ni kwamba sisi watatukomboa gerezani maana tumechoka, tunaiomba serikali iingilie kati suala hili," alisema Nyembela bila shaka, pasi na kutambua kwamba Sheria ya Madini inawataka wawe na leseni ya uchimbaji na pia wawe na makubaliano na mmiliki wa eneo yanakochimbwa madini.

Edger Mwaniti aliwaomba viongozi wa ngazi za juu serikalini wawasaidie kutatua kero hiyo kwa maelezo kuwa viongozi wa ngazi za chini wameshindwa kukabiliana na wawekezaji hao ambao wana nguvu ya kifedha.

Alisema viongozi wa kijiji chao walijaribu kuzungumza na wawekezaji hao ikashindikana na kwamba waliwaomba kama inawezekana wayaache baadhi ya maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo, ombi hilo nalo lilikataliwa.

Ramadhan Ally, mchimbaji mdogo, alisema eneo hilo ambalo wanaondolewa lilikuwa linamilikiwa na babu zao tangu zamani na kwamba wao wamelitumia miaka 26 na hivyo kitendo cha kuvamiwa na wawekezaji kinawazalishia mgogoro.

Alisema mwekezaji huyo hajawahi kuzungumza na wamiliki wa maeneo hayo na badala yake baada ya kupata leseni alianza moja kwa moja kufukia mashimo yao na kuwazuia kufanya shughuli zao hapo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwaoga, Zacharia Mwasile alisema wao wanashindwa kuushughulikia mgogoro huo kwa sababu hawakushirikishwa wakati anapewa leseni ya kuchimba madini kwenye eneo hilo.

Alisema miaka ya nyuma wawekezaji walikuwa wanapitia kwa viongozi wa vijiji, lakini kwa sasa wanapitia ngazi za juu za serikali, jambo ambalo alisema linasababisha ugumu kwenye utatuzi inapotokea migogoro kama huo.

"Kwa sasa kutokana na kukua kwa teknolojia, wawekezaji wanapata maeneo kupitia kwenye mitandao, hivyo sisi viongozi wa vijiji hatuna tena nguvu ya kushughulikia migogoro yao," alisema Mwasile.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Mayeka, alisema ofisi yake iko kwa ajili ya kulinda maslahi ya pande zote mbili; wachimbaji wadogo na wawekezaji.

Alisema mwekezaji anapopata leseni kwenye eneo ambalo wananchi walikuwa wanafanya shughuli zao, ni lazima awalipe fidia na kama hajawalipa fidia serikali ndipo inapoingilia kati.

## 'Wenye uwezo kiuchumi wawasaidie wenye uhitaji'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wenye uwezo kiuchumi jijini Mbeya wameombwa kuwasaidia watu wenye mahitaji maalum ili kupata mahitaji muhimu yanayojumuisha chakula na mavazi.

Ombi hilo lilitolewa jana na viongozi wa Serikali ya Mtaa wa Tonya, Kata ya Ilomba jijini hapa wakati wafanyakazi wa Taasisi ya Tulia Trust walipokabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa wazee wawili ambao hawajiwezi.

Wazee waliokabidhiwa msaada huo ni Mary Mboya ambaye mbali na uzee, pia anakabiliwa na tatizo la macho kupoteza uwezo wa kuona na Daina Nzalanje ambao walipatiwa misaada hiyo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Nichorouus Mihayo alisema wazee na watu wenye ulemavu wana mahitaji mengi ya muhimu kama ilivyo kwa watu wengine.

Alisema wanapokosa mahitaji hayo huwa wanakata tamaa na hivyo maisha yao kuwa magumu zaidi na hivyo akawaomba wadau wengine kuwasaidia.

"Tunamshukuru sana Dk. Tulia kwa kuwaona wazee wetu hawa, lakini anapotoa misaada hii anatupa fundisho na sisi wengine kuwa na moyo wa kujitolea kwa makundi haya," alisema Mihayo.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Dk. Tulia, Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Mbeya Mjini, Clemence Mwandembwa alisema kuwa hivi karibuni Dk. Tulia aliwatembelea wazee hao na kuahidi kuwasaidia.

Alisema misaada iliyotolewa kwa wazee hao ni chakula, nguo na fedha taslimu kwa ajili ya kuhakikisha maisha yao yanaendelea kuwa bora.

"Dk. Tulia alipokuwa kwenye ziara yake kwenye kata hii alikutana na hawa kinabibi wakiwa wamejitwisha kuni, akasimamisha msafara na kuongea nao akawaahidi kwamba atawasaidia. Leo (jana) tumekuja kwa ajili ya kutimiza ahadi hiyo kwa niaba yake," alisema Mwandembwa.

Baada ya kupokea msaa huo, Mary alimshukuru Dk. Tulia kwa kumwona, akisisitiza kuwa maisha yake ni magumu kutokana na tatizo la macho ambalo limekuwa linamsumbua.

Alisema kuwa wakati mwingine amekuwa anakosa chakula kutokana na kutokuwa na kipato cha kumwezesha kununua.

# Wizara yaagiza vijiji vyenye mgogoro mpaka vipimwe upya

**Na Elizabeth John,** MAKETE.

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeagiza vijiji saba vya Halmashauri za Wanging'ombe na Makete mkoani Njombe ambavyo vinagombea mipaka, vipimwe upya ili kutatua mgogoro huo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa wakati wa ziara yake mkoani Njombe, akisema mchakato wa upimaji uliotumika awali haukuzingatia tangazo la serikali la upimaji wa mipaka.

Agizo hilo limekuja kufuatia timu ya wapimaji ramani kutoka wizara hiyo kufika na kufanya tafsiri ya tangazo la serikali lililotumika kuanzishwa wilaya za Makete na Wanging'ombe.

"Mipaka ya vijiji vyote vilivyopimwa irudiwe kupimwa upya kwa kuzingatia matangazo ya mipaka ya wilaya kwa kuwa upimaji wa mwanzo haukuzingatia mipaka ya matangazo ya serikali," alisema Silaa.

Waziri huyo pia aliagiza wananchi wa pande zote mbili waheshimu mpaka wa wilaya hizo kulingana na tafsiri ya matangazo ya serikali ya mipaka kama yalivyotafsiriwa na timu ya wataalam.

Waziri Silaa alisema migogoro ya mipaka isiwaingize viongozi kwenye malumbano ambayo hayasaidii.

"Lakini kubwa ni yale maelezo yote hasa lile nililosema la kupima upya vijiji, nikimwandikia taarifa yangu Mheshimiwa Makamu wa Rais (Dk. Philip Mpango) ninaamini litafanyika kwa haraka kwa sababu tunakwenda kwenye mwaka wa uchaguzi wa vijiji na vitongoji na mitaa, hivyo kila mtu ajitambue alipo," alielekeza.

Awali wawakilishi wa wananchi kutoka katika vijiji vya kata ya Moronga, wilayani Makete pamoja na wanaotoka katika vijiji vinavyounda Kata ya Kipengere wilayani Wanging'ombe walisema kilichokuwa kinasumbua miaka yote ni mkanganyiko kwenye ramani.

"Kwenye ramani kinasoma kingine, kwenye gazeti la serikali kinasoma kingine, mkienda kwenye ardhi mnaoneshwa mahali pengine," alisema Ebrania Mbilinyi.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari alisema serikali imetoa fedha nyingi ili kufanikisha upimaji wa ardhi.

Waziri huyo pia alisikiliza mgogoro wa ardhi kati ya Kanisa la Kiinjili la Kiluteri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kusini na wakazi wa Mtaa wa Lunyanywi na Magoda.

Aliiagiza timu ya wataalam kutoka Wizara ya Ardhi kufika na kufanya kazi ili kubaini ukweli.

"Na timu ikija itaongea na kila mtu.

Ninaagiza ujenzi usimame kwa sababu ni eneo lenye mgogoro, mtu huwa anajenga sehemu yake, na sehemu hii kanisa linasema ya kwake na ninyi mnasema ya kwenu.

Ninaahidi kurudi tena Januari 2024 ili kumaliza mgogoro huu," alisema Silaa.



# Apendekeza dawa kukomesha wanaume wanaokatili watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAROBAINI wa kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto ikiwamo ubakaji na ulawiti visiwani Zanzibar umetajwa.

Mwarobaini huo ni wanaume wahasiwe (kutolewa nguvu za kiume) ili kibakio kisifanye kazi.

Ushauri huo ulitolewa jana na Riziki Pembe Juma, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya uzinduzi wa siku 16 za kupinga vitendo vya udhalilishaji.

"Mimi Riziki ambaye ni mzazi, ushauri wangu njia ya kuhasi wanaume wanaowabaka na kuwalawiti watoto itasaidia sana kutokomeza hivi vitendo. Tungepata kama wanaume watatu wakahasiwa ikawa kama mfano imani yangu kwamba itakua somo na funzo tosha kwa wanaume wengine wenye tabia ya kuwadhalilisha watoto," alisema huku akisisitiza kuwa ushauri wake huo ni kama mzazi na sio waziri.

Alisema hakuna mwanamume hata mmoja anayependa kuwa na uume usiofanya kazi na kukosa nguvu za kiume, lakini kutokana na sheria za nchi hairuhusu jambo hilo ndio maana ina sheria ya kupambana na vitendo hivyo. Aliwataka wanaume wenye hamu ya matamanio kuwafuata wanawake watu wazima kuliko kuwaingilia watoto jambo ambalo linawaathiri na familia zao.

"Wanawake watu wazima tumejaa tele kama mna hamu zenu njooni tuzungumze maana wapo wanawake watu wazima ambao wanatamani kufanyiwa kitendo hicho bure bila ya malipo na wale ambao wanahitaji malipo ni madogo kwanini msiende huko ili kila mmoja akamtosheleza mwenzake kuliko kuwaharibu watoto wetu," alisema.

Hata hivyo, alisema dini ya Kiislamu imeruhusu mwanamume asiyetosheka na mke mmoja anayo nafasi ya kuoa wake wanne ili kutimiza matamanio yao.

Riziki aliitaka jamii kuungana kupiga vita vitendo hivyo kwa sababu Zanzibar bila ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia inawezekana.

Alisema licha ya jamii kuhamasika kuviripoti vitendo hivyo katika vyombo husika, bado watoto na wanawake wanaendelea kudhalilishwa na kasi kubwa hivi sasa ipo kwa watoto wa kiume. Alisema kuendelea kufanyika vitendo hivyo, taifa litapoteza nguvu kazi ya taifa ambayo inategemewa kwa maendeleo ya vizazi vya sasa na vijavyo na wanaofanya vitendo hivyo waripotiwe ili sheria ichukue mkondo wake.

Alisema katika kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili, wizara na wadau mbalimbali watafanya mkutano wa uzinduzi ambao utafanyika Novemba 25, Wilaya ya Mkoani Pemba, kufanya matembezi ya wanaharakati na wanajamii wanayoashiria kuungana katika kupinga vitendo hivyo, maandamano ya wanaharakati na matukio mingine.

Akizungumzia kuhusu tukio la mtoto wa miaka 13 (jina linahifadhiwa) kubakwa na baba yake mlezi alisema mtoto huyo kwa sasa anahifadhiwa na serikali katika nyumba salama na hatua za kisheria zinaendelea ili mtuhumiwa akithibitika achukuliwe hatua za kisheria.

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kwa mwezi wa Oktoba, mwaka huu, jumla ya matukio 199 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa, yakiwa na idadi ya waathirika 199 wa matukio hayo na waathirika wengi wakiwa ni watoto kwa asilimia 78.9, wanawake 16.1 na wanaume asilimia 5.0.

# SMZ, SMT kuendelea kutekeleza mipango ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi, amesema serikali zote mbili zitaendelea kutekeleza kikamilifu dira na mipango ya maendeleo, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025, pamoja na sera na mikakati ya maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi nchini.

Aliyasema hayo jana katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, katika sherehe ya Siku ya Uvuvi Duniani iliyofanyika visiwani humo.

Alisema katika kukuza na kuimarisha minyororo ya thamani ya sekta ya uvuvi na mazao ya baharini, serikali itaendelea kupiga vita uvuvi haramu na kuvitaka vyombo husika kuendelea kuchukua hatua zinazostahik kupiga vita uvuvi huo.

Alisema Siku ya Uvuvi Duniani inatokana na tamko la Umoja wa Mataifa la kushajahisha uvuvi endelevu wenye tija kwa wananchi na serikali zote mbili zitaendelea kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia elimu, nyenzo, mitaji na masoko ili kujipatia ajira na kipato kinachokidhi mahitaji.

Adha, Rais Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kuwapatia vyombo na nyenzo za kisasa zitakazowawezesha kuingia katika uvuvi wa bahari kuu pamoja na kuwawekea miundombinu bora ikiwamo ujenzi wa masoko na mitambo ya kuhifadhia samaki.

Dk. Mwinyi alisema katika kuhakikisha sekta ya uvuvi inafanikiwa zaidi, serikali imejipanga kujenga viwanda vya kusarifu na kuchakata minofu ya samaki na dagaa pamoja na kuwekeza zaidi kwa kuwawezesha wavuvi kufuga na kuzalisha samaki katika bahari na maji baridi.

Alisema kupitia programu ya Uviko- 19 ya uchumi wa buluu kwa Zanzibar, jumla ya boti 577 za uvuvi zimetolewa, 500 wamepatiwa wakulima wa mwani, vifaa vya uvuvi kama mishipi, nyavu, GPS na fish finders, kamba na taitai kwa wakulima wa mwani pamoja na kujengwa kiwanda cha kisasa cha kusarifu mwani. Waziri wa Mifugo na Uvuvi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Abdallah Ulega, alisema wizara zote mbili zitahakikisha zinatoa fursa sawa kwa wavuvi wa pande mbili kwa kuwapatia vitendea kazi ili kuweza kuvua kisasa.

Alisema kwa Tanzania bara zaidi ya wavuvi 197,000 wameshapatiwa leseni za uvuvi wa bahari kuu pamoja na zana zote zitakazowasaidia kuvua kisasa na kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Mkaazi kutoka Shirika la Chakula Duniani (WFP), Sara Golden Gipson, alisema WFP inachangia katika shughuli za maendeo ya uchumi wa Zanzibar hasa katika sekta ya uvuvi sambamba na kuwanyanyua wanawake kiuchumi kwa kuwajengea uwezo pamoja na kuwapatia miradi ya kimaendeleo.

Sara alisema WFP inawasaidia wanawake kupiga hatua za maendeleo kwa kuwatatulia changamoto zinazowakabili katika shughuli zao ikiwamo uhaba wa vitendea kazi hasa kwa wakulima wa mwani pamoja na kuwapatia maboksi ya kuhifadhia samaki kwa muda refu bila kuharibika. Makamu wa Pili alizindua vitabu mbalimbali kikiwamo cha sera ya uchumi wa buluu, mkakati wa uchumi wa buluu, Sera ya Uvuvi, mkakati wa uvuvi, mpango mkuu wa uvuvi na mpango kazi wa ukodishaji wa masuala ya kijinsia katika uchumi wa buluu.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrick Soraga (kushoto), akizungumza katika mdahalo wa uwekezaji wa nyumba za makazi unaolenga sheria mpya za uhamiaji zinazotoa vibali kwa wageni kununua na kuwekeza kwenye nyumba hizo nchini, kabla ya uzinduzi wa miradi mipya ya nyumba za makazi za Moyoni Bay na Mwangani SkyLoft, eneo la Fumba, Zanzibar juzi. Wengine ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa CPS Africa Ltd, Sebastian Dietzold (katikati) na Mhandisi wa Miradi wa CPS, Leander Moons. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Rasilimali Zanzibar zinahitaji kuingizwa kwenye mfumo'

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar ina rasilimali za kutosha kuzalisha fedha nyingi, lakini zinahitaji kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa kiuchumi utakaosaidia ukuzaji uchumi ili kuleta maendeleo ya haraka.

Othman aliyasema hayo jana ofisini kwake Migombani mjini hapa alipozungumza na uongozi wa Taasisi ya Wahasibu, wakaguzi na washauri elekezi wa kodi waliongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa taasisi hiyo, Juma Amour Mohammed, waliofika ofisini kwa Makamu kujitambulisha baada ya taasisi hiyo kuundwa hivi karibuni.

Alisema, kuwapo kwa chombo hicho ni muhimu katika kusimamia maendeleo ya ukuzaji uchumi wa kileo na lazima rasilimali za kifedha zilizopo zikaingizwa katika mfumo mzuri na sahihi ili kuongeza uwezo wa rasilimali fedha zinaopatikana katika biashara na uwekezaji.

Aidha, alisema nchi nyingi duniani zimepiga hatua kubwa ya kiuchumi na kimaendeleo kutokana na kuwapo mifumo na taratibu bora inayowezesha fedha kupatikana kwa wingi kwa vile wawekezaji watajenga imani sahihi na mifumo iliyopo nchini.

Alisema chombo hicho pia ni muhimu kusaidia kuwawezesha wataalamu wa ndani wa kada za fedha, biashara na ukaguzi wanaosimamia vyema taaluma yao kiushindani katika ngazi za kitaifa na kimataifa na nchi kunufaika katika ajira kwa ndani na nje ya nchi.

Aliitaka taasisi hiyo kuwajengea uwezo wanataaluma wao, kwa kuzingatia viwango vya elimu, pia kuthamini wenye ujuzi na maarifa mapana ya kutambua na kumudu vyema majukumu yao kupitia mawanda mapana waliyonayo kuifahamu mifumo na taratibu za dunia za kiuchumi unaolenga ushindani kwenye shughuli za kibiashara na uzalishaji ndani na nje ya nchi.

Akizungumzia suala la taaluma ya kodi, Othman aliutaka uongozi wa taasisi hiyo kuwajenga wanataaluma hiyo katika misingi mipya ya kodi itakayosaidia kuchangia ukuaji wa uchumi kwa haraka kama zilivyoweza kufanikiwa nchi nyingine duniani.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa taasisi hiyo, Juma Amour Mohammed, alisema taasisi hiyo inalenga kuijenga kada hiyo kufuata na kuzingatia maadili ya kifedha ambayo yameonekana kupotea.

Alisema, watendaji wengi walikosa kujiamini na kutokuwapo uadilifu katika utendaji wa majukumu yao ikiwamo uandishi wa ripoti za kifedha na kuwapo kwa taasisi hiyo kutawezesha kusimamia vyema maadili na taaluma ya kiuhasibu Zanzibar.



Takataka zilizosombwa na maji ya mvua zikiwa ndani ya mtaro, Mwenge, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, kutokana na utupaji holela wa taka katika eneo hilo, ambalo ni maarufu kwa shughuli za wafanyabiashara wadogo 'machinga'. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Halmashauri zakwepa kuingia kwenye mfumo mpya ununuzi

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imebainisha kuwa hadi sasa, halmashauri 115 hazijawasilisha mipango yao ya ununuzi katika Mfumo mpya wa Ununuzi wa Umma (NeST) huku sita pekee sawa na asilimia 3.3 ndio zinatumia vizuri mfumo.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka hiyo imesema kuwa kupitia sheria mpya ya ununuzi wa umma iliyopitishwa na Bunge hivi karibuni, inayo meno zaidi kuchukua hatua kwa kuwapeleka mahakamani na adhabu zake ni kulipa faini ambayo si chini ya Sh. milioni 10 au kifungo cha miaka saba gerezani au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Eliakim Maswi aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wakurugenzi wa halmashauri zote nchini yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema halmashauri zingine 69 zimewasilisha mipango ya ununuzi katika mfumo wa ununuzi na kati ya hizo, sita tu ndizo zinazotumia kikamilifu mfumo huo.

"PPRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI waliandaa mafunzo kwa mikoa yote 26, tuliomba halmashauri zifundishwe ambapo watumishi 1,687 walipata elimu hiyo, tumekutana na TAMISEMI kuona kuna umuhimu wa kukutana na wakurugenzi ambao ni wasimamizi wakuu.

"Kwa mujibu wa sheria na kama hawatataka kutumia mfumo, maana yake wanatakiwa kuadhibiwa kwa kutotumia mfumo. Bahati nzuri tumeanzishiwa kitengo maalum cha kushtaki ndani ya mamlaka kwa watu wasiotaka kutumia.

"Lakini halmashauri za mjini Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya hazijawahi kutumia mfumo. Kwa hiyo, zilizofanya vizuri sana ni pamoja na Ngara, ambayo imetoa mikataba 20 mpaka jana.," alisema.

Alitaja halmashauri nyingine zilizofanya vizuri ni Nyan'gwale ambayo mpaka jana imetoa zabuni 11, Misenyi zabuni sita, Makete zabuni mbili na Temeke imetoa zabuni moja ya zaidi ya Sh. milioni 730, Manispaa ya Songea ilitoa zabuni moja.

"Tuna halmashauri 115 ambazo kimsingi hazina habari kama kuna kutumia mfumo, lakini tuna halmashauri tisa ambazo hazijui kabisa kama kuna suala la mfumo kwa maana kwamba hata kuingia kwenye mfumo hawajawahi kuingia.

"Sasa sielewi kama hawakuhudhuria mafunzo, lakini kwenye orodha ya mafunzo walihudhuria lakini hata kuanza hizi zingine 106 zimeanza lakini hazijatumia.

"Kwa mfano, Ubungo, Dar es Salaam idara mbili hazijakalimika na hilo sio jukumu letu kukamilisha, sasa halmashauri tisa hazijui kama kuna mfumo wa ununuzi wa umma.

"Hii ni hatari na ombi langu kwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais -TAMISEMI, ninaomba unisaidie kwa sababu hatuwezi kwenda hivi.

"Unajua serikali bwana ni raha sana hatuwezi kubembelezana na kwa bahati nzuri sheria yetu ya ununuzi wa umma tuliyopitisha juzi imetupa madaraka ya ajabu kwelikweli PPRA, nisipokuhamishia nimekupenda sana nataka nikupeleke mahakamani na utalipa si chini ya Sh. milioni 10 au miaka saba jela au vyote viwili,"alihadharisha.

Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Serikali za Mitaa, Sospeter Mtwale aliwataka wakurugenzi hao kuzingatia waraka, miongozo na sheria za PPRA ili mfumo utumike ilivyokusudiwa.

"Kwa kuwa mfumo huu utatumika maeneo yote ya serikali, hakikisheni maofisa masuhuli wote wanatekeleza kazi zao kwa weledi, na kama kuna mahali una matatizo zisemwe ili ufanyiwe maboresho na kuwapo ufanisi zaidi," alisema.

# TRA yafadhili ujenzi wa madarasa

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imefadhili ujenzi wa madarasa mawili na ununuzi wa madawati 100 katika Shule ya Msingi Kisarawe II iliyoko Manispaa ya Kigamboni ikiwa ni shukrani ya mamlaka hiyo kwa walipakodi.

Akizungumza jana alipokabidhi ufadhili huo, Naibu Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa, Eunice Liheluka, alisema TRA imetumia Sh. milioni 50 katika mradi huo.

Alisema lengo la ufadhili ni kushiriki katika kugusa maisha ya watu kupitia huduma za kijamii kwa kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha elimu.

"Niwaombe wanafunzi na walimu mtunze madarasa haya pamoja na madawati ili yatumike kwa muda mrefu. Fedha tulizotoa ni sehemu ya kile kidogo tunachopokea kutoka serikalini, nasi tukaona turudishe kwa umma," alisema.

Akipokea ufadhili huo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Upendo Mahalu, aliishukuru TRA na kuyaomba mashirika na kampuni zingine kujitokeza kusaidia ujenzi wa miundombinu ya shule.

"Kama mnavyofahamu wilaya yetu bado ni changa ina mahitaji mengi. Tuna upungufu wa madarasa na madawati japokuwa tumepata fedha kupitia mradi wa Boost kwa ajili ya shule za msingi, bado mahitaji ni makubwa," alisema.

Alibainisha kuwa wana uhitaji wa madarasa zaidi ya 1,000 na madawati kwa shule za msingi na sekondari.

Mkuu wa Shule ya Msingi Kisarawe II, Joseph Kavishe, alisema shule hiyo ina wanafunzi 1,408 na ina upungufu wa madarasa 18.

"Mradi huu umetusaidia kupunguza mlundikano wa wanafunzi darasani. Madawati 100 yatawasaidia wanafunzi 300 waliokuwa wanakaa chini, sasa watakaa kwenye madawati. Bado tuna upungufu wa madawati 168," alisema.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
WILAYA YA MOROGORO
LILILOPO MOROGORO

MAOMBI MADOGO NAMBA 63 YA 2023

TATU RAJABU MOHAMED (Suing through Power of attorney of FATMA SAID KIBWANA)........MLETA MAOMBI

DHIDI YA

JULIUS PETER SHAYO,ABIYA YONA MATHIAS,MUSSA TINDA.............WAJIBU MAOMBI
AMINA RAMADHANI SHADA.........NECESSARY PARTY

WITO/KUITWA SHAURINI KWA
AMINA RAMADHANI SHADA

Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza za Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 30/11/2023 mbele ya mwenyekiti M.KHASIM wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilzwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 20 Mwezi November, 2023.

M. KHASIM
MWENYEKITI

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

LAMECK JOHN KAAYA
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA NOAH** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T720 BXN**, ENGINE NAMBA **257911087** CHASSIS NAMBA **sr500090121** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE T AARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA
**PHQ/ARU/ARU 6708/2023**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE

Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa mirathi Na....1778/2023

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU ALLY M. MOHAMED WA TABATA

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA
NA MAJUTO MWINYIMJA ABDALA

TANGAZO
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU

NAFASI ZA KAZI

Ualimu Masomo ya **Hesabu, Science, Kiswahili na Kiingereza.**
Pia wanatakiwa walimu Wastaafu isizidi miaka mitatu (3) iliyopita kwa ajili ya ukaguzi.

SIMU: 0783 298 900

KATIKA MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI
MWANZA

SHAURI LA UTEKELEZAJI NA. 38 YA 2022

WANKURU MARWA MASWI ..................................MWOMBAJI

DHIDI YA

END TIME CHURCH OF GOD MINISTRY NA WENZAO 8....WAJIBU MAOMBI

Kwa:
ONESMO BALIKULE.........................MJIBU MAOMBI NAMBA2
DR. MWIJARUBI..............................MJIBU MAOMBI NAMBA 3
ADAM IKWADU.................................MJIBU MAOMBI NAMBA 4
LUCAS MBOGOYO............................MJIBU MAOMBI NAMBA 6
ESTHER DEUS..................................MKIBU MAOMBI NAMBA8

POPOTE MLIPO.
KUITWA SHAURINI

Fahamu kwamba, shauri tajwa hapo juu ambalo nyinyi ni WAJIBU MAOMBI limepangwa kusikilizwa mbele ya mahakama hii tarehe 27/11/2023 saa 3:00 asubuhi, mbele ya **MHE. C.M KISONGO MSAJILI**. Hivyo unatakiwa kuhudhuria Mahakama wewe mwenyewe au mwakilishi wako siku hiyo bila kukosa. Kutohudhuria kwako kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo. Imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 21 Mwezi NOVEMBA, 2023.

NAIBU MSAJILI
MWANZA.

# Utekelezwaji usitishwaji mapigano waingia utata

**TEL AVIV, Israel**

MPANGO wa kusitishwa mapigano kwa siku nne kati ya Israel na Hamas ili kuruhusu msaada kuingia Ukanda wa Gaza na kuachiliwa baadhi ya mateka wanaoshikiliwa umekuwa na utata baada ya Israel na Hamas kutofautiana muda kamili wa kuanza kwake.

Wakati Hamas awali walisema mpango huo ungeanza kufanya kazi Alhamisi saa nne kamili asubuhi. Lakini Israel ilisema pengine ungeanza leo.

Mshauri wa usalama wa taifa Tzachi Hanegbi alisema mawasiliano kuhusu kuachiwa kwa mateka wao yanaendelea kupiga hatua. Hata hivyo hajasema ni wakati gani Israel itasitisha mashambulizi yake ya anga na ardhini katika eneo hilo.

Wakizungumza mjini Tel Aviv katika kikao cha pamoja cha waandishi wa habari Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu, waziri Benny Gantz na Waziri wa Ulinzi Yoav Gallant, waliapa kuwaleta nyumbani mateka wote na kuwaangamiza wanamgambo wa Hamas.

Netanyahu alisema kuwa vita hivyo vitaendelea hadi watakapoyatimiza malengo yao.

Alisema shirika la Msalaba Mwekundu litaruhusiwa kuwatembelea mateka watakaobaki Ukanda Gaza na aliongeza kuwa wakati mwingine kazi yake inahitaji maamuzi magumu.

Waziri Gallant alisema ana matumaini ya dhati kuwa makubaliano ya kubadilishana mateka yatatekelezwa kutokana na matokeo ya mazungumzo yanayoendelea yatayoonekana katika siku chache zijazo.

Chini ya mpango huo, mateka 100 wataachiwa kutoka Gaza kwa kubadilishana na wafungwa 300 wa Kipalestina wanaoshikiliwa nchini Israel.

Aidha, malori yaliyobeba misaada ya dharura yataruhusiwa kuingia Ukanda wa Gaza ambako hakuna chakula, maji, umeme na dawa na vifaa vya matibabu. Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuwashughulikia Watoto (UNICEF) Catherine Russell aliuita Ukanda wa Gaza uliozingirwa na majeshi ya Israel kuwa ni sehemu hatari kwa mtoto kuishi.

Alisema makubaliano yaliyofikiwa ya kusitisha mapigano kati ya Israel na Hamas hayatoshi kuyaokoa maisha yao.

Russell aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuwa zaidi ya watoto 5,000 wameripotiwa kuuawa tangu shambulizi la Hamas dhidi ya Israel Oktoba 7, ikiwa ni asilimia 40 ya vifo vyote mpaka sasa.

Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Uingereza David Cameron alijadiliana na viongozi wa nchi za Kiarabu na zenye Waislamu wengi kuhusu suluhisho la kisiasa kuelekea kuachiwa huru mateka wote.

Taarifa ya serikali ya Uingereza ilisema wanadiplomasia hao waliangazia jinsi ya kusaidia kutekelezwa kwa makubaliano hayo.

Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Saudi Arabia, Jordan, Misri, Mamlaka ya Palestina, Uturuki, Indonesia na Nigeria Pamoja na Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kirabu na Balozi wa Qatar, walihudhuria mkutano huo.

Wakati huo huo, watu 52 wameuawa wakati muda wa usitishwaji mapigano ukisubiriwa.

Shirika la habari la Palestina (Wafa) limeripoti juu ya mauaji hayo baada ya ndege za Israel kushambulia kambi ya wakimbizi.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Mamlaka ya Ndani ya Palestina, Riyad al-Maliki, alisema watu hao waliouawa katika kambi ya wakimbizi ya Jabalia kaskazini mwa Ukanda wa Gaza Jumatano asubuhi walikuwa wa familia moja.

"Ni asubuhi tu ya leo, kutoka kwa familia ya Qadoura huko Jabalia, watu 52 wameangamizwa kabisa, wameuawa," alisema wakati akisafiri kuelekea Uingereza.

Mamlaka ya Ndani ya Palestina ina makao yake katika Ukingo wa Magharibi unaokaliwa na ni tofauti kabisa na Hamas.

**DW**




Kiongozi wa chama cha Economic Freedom Fighters (EFF) nchini Afrika Kusini Julius Malema akiondolewa kwa nguvu kutoka ndani ya ukumbi wa bunge baada ya wabunge kutoka chama hicho kupiga kura ya kumzuia kuhudhuria vikao kwa mwezi mmoja.**PICHA:BBC**

# Watu 50 wafa kwa njaa Ethiopia

**ADDIS Ababa, Ethiopia**

ZAIDI ya watu 50 wamefariki dunia katika maeneo ya kaskazini mwa Tigray na Amhara nchini Ethiopia kutokana na njaa iliyosababishwa na ukame.

Maofisa wa eneo hilo wameiambia BBC kuwa watu 46 walikufa baada ya kukimbia makazi yao kwa sababu ya ukame.

Vifo hivyo vilitokea katika mji unaoitwa Yechila, mkuu wa ofisi ya Tigray, Gebrehiwot Gebregziabher alisema.

Katika eneo jirani la Amhara la Wag Hemra, takriban watu sita na ng'ombe 4,000 wamekufa kwa kukosa chakula uliosababishwa na ukame.

Kwa zaidi ya miezi mitano, Marekani na Umoja wa Mataifa walikuwa wamesitisha msaada wa chakula kwa Ethiopia kufuatia madai ya wizi.

Hali hiyo inazidisha mateso ya kibinadamu nchini humo inayotokana na vita na hali mbaya ya hewa iliyowaacha mamilioni ya watu wakitegemea misaada.

Maeneo ya kaskazini mwa Ethiopia yanakabiliwa na hali ya ukame mkali, maeneo ya kusini na mashariki mwa nchi hiyo yanatarajiwa kukumbwa na mafuriko kutokana na mvua kubwa kunyesha.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, zaidi ya watu 40 wamefariki katika wiki za hivi karibuni kutokana na mafuriko na maporomoko ya ardhi, wengi wao wakiwa katika eneo la mashariki mwa Somalia.

**BBC**

## Wawekezaji Zanzibar wafurahia mabadiliko ya Sheria ya Uhamiaji

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Mudrick Soraga, amesema ipo haja sheria mpya uhamiaji kuhimiza uwekezaji kwa wageni katika soko la nyumba za makazi Zanzibar.

Kiongozi huyo aliyasema hayo jana wakati wa uzinduzi wa miradi ya nyumba za makazi eneo la Moyoni Bay na Mwangani SkyLoft chini ya kampuni ya CPS Afrika.

Alisema kuwa kabla ya mabadiliko, mtu wa nje akitaka kununua nyumba kupata vibali inakuwa ngumu, lakini kwa sasa mtu akiwekeza makazi, anapata kibali cha kuishi nchini miaka mitano.

Waziri Soraga alisema kutokana na mabadiliko hayo ni wakati muhimu katika kutetea uwekezaji wa kigeni visiwani humo ambao utachochea ukuaji sekta ya nyumba.

Aliwatoa hofu wawekezaji wa kigeni kuhusu usalama na uhakika wa uwekezaji Zanzibar.

"Kitendo hiki kinaonesha dhamira yetu isiyoyumba katika kuhakikisha mazingira ya uwekezaji yanakuwa salama na ari ya serikali katika kulinda maslahi ya wawekezaji wa kigeni.

"Sheria mpya ya Uhamiaji kuhusu wanunuzi au wawekezaji wa nyumba za makazi kuwa na vibali vya ukazi kwenye nchi hii ni jambo la kihistoria ambalo linakwenda kufungua soko la nyumba za makazi na pia kufungua soko la utalii utaotanua wigo wa wawekezji ambao wanaingia nchini," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa CPS AFRICA, Sebastian Dietzold, alipongeza uamuzi wa serikali kufanya mabadiliko ya sheria hiyo kwa kutoa vibali vya kuishi kwa wanunuzi wa nyumba wanaowekeza zaidi ya Dola za Marekani 100,000.

"Tumefurahishwa na mpango huo wa serikali," alisema na kusisitiza uwezeshaji unaowaletea wateja na mashirika ya diaspora wanaotaka kujihusisha na soko la nyumba za makazi Zanzibar.

Alisema mabadiliko hayo yatawakaribisha watalii duniani watakaotaka kununua nyumba nchini na kuongeza kukuza uchumi ambao kwa Zanzibar imechukuliwa kwa uzito wake.

"Tuna miradi zaidi ya 36 ya nyumba za makazi na wenzetu wa CPS Africa wamewekeza zaidi ya Dola milioni 300, ni sekta inayokua kwa kasi kubwa na kuinua uchumi na kuongeza mnyororo wa thamani nchini," alisema.

# SHABIKI AVUNJA MCHEZO ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MCHEZO wa Ligi Kuu Zanzibar kati ya Zimamoto SC na Kundemba FC uliochezwa juzi kwenye uwanja wa Mau A ulishindwa kuendelea baada ya shabiki kumshambulia mwamuzi msaidizi.

Shabiki huyo anayedhaniwa kuwa ni wa klabu ya Kundemba aliingia uwanjani wakati mchezo huo ukiendelea na kumshambulia mshika kibendera na kupelekea mchezo huo kusimama.

Mchezo huo ulivunjika katika dakika nane za nyongeza wakati timu hizo zikiwa zimeshafungana mabao 2-2.

Mchezo huo tangu unaanza mashabiki wa timu ya Kundemba mara nyingi walikuwa wakimtupia lawama mshika kibendera huyo kwa madai kuwa hatoi maamuzi sahihi.

Akizungumza na Nipashe katibu wa Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya, Omar Sheha alisema wanatarajia kutoa maamuzi ya mchezo huo ndani ya masaa 72 kama kanuni inavyoeleza.

Alisema tayari kamati hiyo imeshaanza kuchukua hatua kwa kupitia ripoti ya mwamuzi wa mchezo huo na kukusanya taarifa za mchezo huo kutoka kwa wasimamizi na walinzi ambao walikuwa upande wa mshika kibendera huyo aliyeshambuliwa.

Alisema vilabu vinatakiwa kuwadhibiti mashabiki wao ili kuepuka vitendo vyovyote vya fujo ambavyo vinaweza kutokea kabla na baada ya mchezo.

"Kanuni ipo wazi kama hujaridhika zipo njia za kupita na kuleta malalamiko yako ofisini badala ya kujichukulia sheria mkononi, hivyo kamati itatoa maamuzi ya mchezo huo kwa mujibu wa kanuni inavyoeleza ndani ya masaa 72"alisema kiongozi huyo.

Tukio hilo linakuwa la kwanza kwa Ligi kuu ya Zanzibar kwa kuvunjika mchezo kabla ya wakati wake tangu kuanza kwa msimu huu wa 2023/2024.



Wachezaji wa timu ya taifa ya wanawake 'Twiga Stars' wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mchezo wao wa kufuzu fainali za Afrika dhidi ya Togo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Prisons yampa rungu kocha mpya

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa klabu ya Tanzania Prisons umesema umesitisha mchakato wa usajili waliokuwa wakifanya mpaka pale watakapopokea mapendekezo ya kocha wao mpya Hamad Ally.

Jana, Tanzania Prisons ilimtangaza Ally kuwa kocha mpya wa timu hiyo akichukua nafasi ya Fred Felix 'Minziro' ambaye amefungashiwa virago kwenye klabu hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Ajabu Kifukwe alisema wameriridhishwa na uwezo wa kocha huyo mpya na sasa wamempa rungu la kpendekeza wachezaji wa kusajili na kuwaacha kwenye dirisha dogo la usajili la Januari.

Alisema awali walipokea mapendekezo ya usajili kwa kocha aliyeondoka na walianza kufanyia kazi baada ya kupatikana kwa mwalimu mpya wamesitisha na kumpa kipaumbele kocha wao mpya.

"Tulianza kufatilia baadhi ya wachezaji kwa kutaka kuongeza nguvu lakini zoezi hilo tumelisitisha, na tumempa nafasi Kocha Hamad kuangalia kikosi chake na wapi anatakiwa kuboresha.

"Tutashirikiana na kumueleza mapendekezo ambayo tumepewa na kocha wa awali (Minziro) ili kuona ni wapi naye anataka kufanya maboresho baada ya kuona kikosi cha timu yetu," alisema Kifukwe.

Aidha, aliongeza kuwa wanaimani kubwa na Hamad kuwafikisha kwenye malengo yao ya kufanya vizuri na kuwaondoa kwenye nafasi ya 14 wanayoishika sasa.

## Wachezaji Gofu wajigamba NCB Open 2023

**Na Mwandishi Wetu**

WACHEZAJI Gofu wa kulipwa na ridhaa nchini wamedhamiria kufanya vizuri katika michuano ya NCBA Tanzania Open 2023 iliyoanza jana kwenye Uwanja wa Kili, Arusha.

Zaidi ya wachezaji 200 wa kulipwa kutoka nchi za Malawi, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Rwanda, Burundi, Zimbabwe, Zambia na wenyeji Tanzania wanachuana kuwania taji la mashindano hayo ya wazi.

Miongoni mwa wachezaji wa gofu wa kulipwa wanaoshiriki katika michuano hiyo ni pamoja na Nuru Mollel, Fadhil Nkya, Isaac Wanyeche, Abdallah Yusuf na Frank Mwinuka huku wachezaji wa ridhaa ni pamoja na Ally Isanzu, Isihaka Daudi, George Sembi na Michael Masawe.

Mmoja wa wachezaji kutoka Tanzania, Isaac Mollel, alisema kuwa wamejipanga vizuri kuhajkikisha wanaipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye mashindano hayo.

## BMT yaishukuru ICRC kwa baiskeli

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo Tanzania (BMT) limeishukuru taasisi ya 'International Committee of the Red Cross ' (ICRC) kwa msaada wa Baiskeli 12 walizozitoa kwa Chama cha Mpira wa Kikapu kwa watu wenye ulemavu nchini (TWBA).

ICRC imetoa msaada wa baiskeli hizo kwa TWBA ikiwa ni muendelezo wa kuwaunga mkono katika kuendeleza mchezo huo wa mpira wa kikapu.

Hii ni mara ya tatu kwa ICRC kutoa msaada wa aina hiyo kwani tayari wametoa idadi hiyo ya baiskeli Zanzibar na mkoani Kilimanjaro.

Akizungumza na waandishi wa Habari Jana, Katibu Mtendaji wa BMT, Neema Msitha alisema kuwa anawashukuru TWBA na ICRC kwa ushirikiano wao wa kuinua mchezo wa kikapu kwa watu wenye ulemavu.

"Viongozi wanapaswa kuwa wabunifu kwa kutafuta wadau ambao watawaunga mkono kila siku, narudia michezo ni gharama sana hivyo inahitaji uwekezaji ili upate kitu kizuri.

"Hii si mara ya kwanza au ya pili tunaona TWBA wanapokea baiskeli hizi, ni jitihada za viongozi wao kujipambanua na kujua nini wanataka ili kuuendeleza mchezo huu wa kikapu," alisema Neema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MAN UNITED KUUZA WACHEZAJI
KLABU ya Manchester United inajiandaa kuliuza kundi jingine la wachezaji mwaka 2024, huku zaidi ya wachezaji 10 wakitarajiwa kuondoka katika madirisha mawili yajayo ya uhamisho. **(Mail)**

### HAALAND ASHAWISHIWA
KLABU ya Manchester City inajaribu kumshawishi mshambuliaji Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23 kusaini mkataba mpya, lakini makubaliano na mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway bado hayajakamilika. **(TeamTalk)**

### LEWIN AFUATILIWA
KLABU ya Newcastle United inafuatilia hali ya Dominic Calvert-Lewin kule Everton huku mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 26 akiwa kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kuwindwa msimu ujao. **(TeamTalk)**

### ANDRE SAFI FULHAM
KLABU ya Fulham imewazidi Liverpool na Manchester United katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Fluminense na Brazil, Andre mwenye umri wa miaka 22, huku mshambuliaji wa Wolfsburg, Jonas Wind mwenye miaka 24 pia akiwa miongoni mwa walengwa wa klabu hiyo. **(Standard)**

### CHELSEA YAWINDA NYOTA
CHELSEA inawafuatilia mshambuliaji wa Feyenoord na Mexico, Santiago Gimenez mwenye umri wa miaka 22 na winga wa Real Betis kutoka Senegal, Assane Diao mwenye miaka 18. **(Football Transfers)**

### ARSENAL KUSAJILI STRAIKA
KLABU ya Arsenal imeamua kusajili mshambuliaji mpya mwaka 2024 - lakini biashara hiyo inaweza kusubiri hadi dirisha majira ya joto. **(Football Insider)**

### JORGINHO BASI TENA
MAZUNGUMZO ya kiungo wa kati wa Italia, Jorginho ya kuongeza mkataba na Arsenal yamekwama, kwa mujibu wa wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. **(Mail)**

### CACERES KIPAUMBELE
MLINZI wa Club America na Uruguay, Sebastian Caceres mwenye umri wa miaka 24 ameibuka kama usajili wa kipaumbele wa Tottenham Hotspur katika dirisha la uhamisho la Januari. **(football.London)**

### BADIASHILE ASAKWA
KLABU ya AC Milan ina nia ya kutaka kumnunua kwa mkopo beki wa Chelsea, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 22 raia wa Ufaransa, klabu hiyo ya Italia pia itawasiliana na Arsenal kuhusu kupatikana kwa mlinzi wa Poland, Jakub Kiwior mwenye umri wa miaka 23. **(Calciomercato)**

### CHOLABAH KUUZWA
CHELSEA iko tayari kumuuza mlinzi wa England, Trevoh Chalobah mwenye umri wa miaka 24. **(Football.London)**

### SPURS KUCHUNGUWA
CHAMA cha soka cha England (FA) kimethibitisha kuwa kinachunguza madai ya ukiukwaji mkubwa wa sheria za mawakala katika uhamisho unaohusisha Tottenham Hotspur na Portsmouth na mshambuliaji wa zamani wa England, Jermain Defoe. **(Times)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DECO: HAKUNA MBADALA WA GAVI BARCELONA

**Amepuuza uvumi wote kuwa klabu hiyo ina mpango wa kutafuta...**

**BARCELONA, Hispania**

MKURUGENZI wa michezo wa Barcelona, Deco amekiri kuwa haitawezekana kuziba nafasi ya Gavi ambaye ni majeruhi kwenye soko la usajili na akapuuza uvumi kuwa klabu hiyo

itatafuta kiungo mpya Januari.

Msimu wa Gavi wa 2023/24 huenda ukawa umemalizika baada ya kuumia wakati wa ushindi wa 3-1wa wa timu yake ya taifa ya Hispania nyumbani dhidi ya Georgia katika mechi ya kufuzu Euro 2024 Jumapili.

Ripoti zinadai kuwa Hispania wanasita hata kumwita Gavi tena hadi 2025 baada ya kuikasirisha Barcelona kwa kumchezesha kwenye mechi ambayo haikuwa na umuhimu mkubwa.

Barca wamemshutumu kocha wa Hispania, kumchezesha kupita kiasi kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, huku kiungo huyo akicheza michezo 111 kati ya 121 ambayo wamecheza tangu alipoanza mechi yake ya kwanza mwaka 2021.

Huku Gavi sasa akitarajiwa kukaa nje ya uwanja kwa muda mrefu, Barcelona wamepigiwa upatu kujaribu kutafuta mbadala wake wa muda katika dirisha la usajili la Januari, huku Thiago Alcantara wa Liverpool na Giovani Lo Celso wa Tottenham Hotspurs wakiwa miongoni mwa viungo wanaohusishwa na uhamisho wa kwenda Katalunya.

Lakini akizungumza na EFE, Deco alisisitiza kuwa hakuna mpango wa kuchukua nafasi ya Gavi moja kwa moja na usajili mpya.

"Gavi ni mchezaji ambaye hawezi kuwa na mbadala. Hakuna mchezaji anayepatikana sokoni kufanya kazi yake, si kwa mawazo yake, wala kwa uwezo wake," alisema Deco.

"Kujadili kuhusu kuchukua nafasi ya Gavi ni kosa, ni kosa kufikiria kwamba tutatafuta mchezaji wa kuchukua nafasi yake. Hatutampata.

"Hatutakuwa na wazimu kwa kuumia kwa Gavi. Inasikitisha kwake, kwetu kama klabu, lakini hatutapata mbadala wake.

"Tuna huzuni sana, lakini nina uhakika kwamba atarudi kwa nguvu, atapona, ni mtoto mdogo ambaye ana nguvu za ajabu, na tunachofanya ni kumsaidia kurejea kwa nguvu, hilo ndilo jambo muhimu zaidi."

Barcelona watarejea kwenye mechi ya LaLiga bila Gavi kesho Jumamosi kwa safari ya kwenda kwa Rayo Vallecano.

# GRIEZMANN HANA MPANGO KUONDOKA ATLETICO




**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Atletico Madrid na timu ya taifa ya Ufaransa, Antoine Griezmann inaelezwa hana mpango wa kutimka ndani ya klabu hiyo baada ya kuhusishwa na kujiunga na Manchester United.

Griezmann amekua akihusishwa na kujiunga na Man United, lakini vyanzo vya ndani kutoka klabu ya Atletico Madrid vinaeleza kuwa nyota huyo hana mpango wa kutimka klabuni hapo.

Inafahamika kuwa mshambuliaji huyo amewekeza akili yake ndani ya viunga vya dimba la Wanda Metropolitano baada ya kukataa ofa ya kujiunga klabu mbalimbali za Saudia, na hivyo suala la kujiunga na Man United ni jambo ambalo sio rahisi.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa amekua kwenye kiwango kizuri msimu huu ndani ya Atletico Madrid, jambo ambalo limeifanya klabu ya Man United kufukuzia saini ya mchezaji huyo.

Griezmann ni wazi kuwa hana mpango wa kuondoka ndani ya klabu ya hiyo na kutimkia timu yeyote.

# Jesus: Kufunga siyo nguvu yangu tena

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Gabriel Jesus, amekiri kwamba kufunga mabao si "nguvu"yake tena baada ya kushindwa kuifungia Brazil katika mechi yao ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Argentina, Jumatano.

Licha ya kuumia kwenye mapumziko ya Novemba, Jesus alicheza dakika zote 90 za kichapo cha 1-0 cha nchi yake dhidi ya wapinzani wao Argentina.

Jesus hajaifungia Brazil bao tangu mechi ya kirafiki dhidi ya Korea Kusini Juni 2022, ambapo pia ni bao pekee la kimataifa alilofunga tangu Copa America 2019.

Akiwa amefunga mabao mara 18 katika mechi 35 za kwanza za wakubwa, bao hilo la Korea Kusini ndilo pekee katika mechi 29 zilizopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 hajawahi kuwa mfungaji mabao mara kwa mara katika maisha yake yote.

Ingawa alianza kwa kishindo katika miezi yake ya kwanza barani Ulaya, idadi yake bora zaidi katika kampeni moja ya Ligi Kuu inabakia kuwa ile ya mabao 14 aliyoifungia Manchester City msimu wa 2019/20.

Ni mara mbili pekee katika misimu saba kamili tangu aondoke Brazil ambapo Jesus amefunga mabao zaidi ya 20 na hajawahi kuwa juu zaidi akiwa ya mabao 23.

Akiwa na majeraha mwaka wake wa kwanza na Arsenal msimu wa 2022/23 alifunga mabao 11 katika michuano yote.

"Kuna mambo yalinisumbua sana baada ya kombe la dunia 2018. Nilikuwa mdogo, nilikuwa na mawazo tofauti, leo mimi ni mtu mzima, msomi zaidi, mtu wa familia, naelewa soka ni kipaumbele kwangu, na najua nahitaji kuwa vyema ili kufanya vyema niwezavyo, hasa katika timu ya Brazil," alisema mchezaji huyo akieleza kwa vyombo vya habari vya nchini humo baada ya mechi ya Argentina.

"Kuna vitu siwezi kuvidhibiti, nafanya mazoezi, natafuta, najaribu, nahama, naisaidia timu, naamini sio nguvu yangu tena kufunga."

# Martinez kurejea dimbani karibuni

**MANCHESTER, England**

MLINZI wa Manchester United, Lisandro Martinez juzi alionekana kwenye mazoezi ya Klabu hiyo pale Carrington na sasa ana uwezekano wa kurudi dimbani.

Martinez amekua na majeraha tangu Septemba katika mchezo dhidi ya Bayern Munich, lakini anatarajiwa kurejea hivi karibuni baada ya kuonekana mazoezini.

Beki huyo wa kimataifa wa Argentina ameonekana Carrington, lakini hakua anafanya mazoezi na wenzake.

Alikua anafanya mazoezi ya peke yake na hii inaonesha amepata nafuu kwa kiwango kikubwa.

Kwa kawaida wachezaji wenye majeraha huwa hawafanyi mazoezi na kama wataanza kufanya basi watafanya mazoezi ya ndani.

Lakini kuonekana kwake hadharani kuna maanisha kwamba, anauwezekano mkubwa wa kurudi dimbani hivi karibuni.

Martinez alikua msaada mkubwa kwa Man United msimu uliomalizika akicheza kwenye kiwango kikubwa.

Hivyo kama atarejea hivi karibuni ataenda kuipa nguvu klabu hiyo ambayo kwa sasa imeonekana kukosa nguvu na kupata matokeo mabaya.



HABARI MICHEZO

# DITTO AIDAI FIDIA MULTI CHOICE TANZANIA

**Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Lameck Ditto ameiomba Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam iamuru Kampuni ya MultiChoice Tanzania imlipe fidia ya Sh. 6/- Bilioni kwa kutumia wimbo wake kwenye matangazo yao ya kibiashara bila ridhaa yao.

Ditto ambaye jina lake halisi ni Dotto Bernard Bwakeya amedai Mahakamani hapo, kampuni hiyo ilitumia wimbo wa Nchi Yangu aliodai ni wake kwenye matangazo yao ya biashara pasipo kuwasiliana naye na kukubaliana.

Pia ameiomba Mahakama iamuru alipwe Milioni 200 kutokana na madhara ya jumla, pia alipwe riba ya asilimia 25 tangu siku alipofungua shauri hilo.

Ditto alitoa ushahidi wake kwa saa sita, mbele ya jaji Hamidu Mwanga wa Mahakama hiyo katika kesi ya madai, akiilalamikia MultiChoice Tanzania Limited kutumia wimbo huo kwenye matangazo yao ya biashara kipindi cha Kampeni ya Afcon 2019.

Akiwasilisha ushahidi wake, alidai, MultiChoice imempora fursa ya kunufaika na kazi yake kupitia wimbo huo.

Miongoni mwa vielelezo alivyoviwasilisha Mahakamani hapo ni mawasiliano ya barua pepe (email) ambayo alidai alifowadiwa na Emmilian Mallya aliyekuwa mratibu wa Tamasha la Urithi ambayo ilionyesha ushiriki wa wimbo wake huo kwenye Tamasha hilo.

"Mheshimiwa jaji, huu ni wimbo wangu na mimi ndiye mmiliki, niliutunga wa kwanza nikaimba mwenyewe, nikaombwa nitunge wa pili kwa ajili la Urithi ambao umeimbwa na wengi," alidai Ditto wakati akitoa ushahidi wake.

Awali, Wakili anayeiwakilisha MultiChoice, Mlano Mlekano alidai walitumia Wimbo wa Nchi Yangu, lakini sio huo unaolalamikiwa na mdai.

Hata hivyo, Jaji Hamidu alisema, kinacholalamikiwa Mahakamani hapo ni Wimbo wa Nchi Yangu uliotumiwa na kampuni hiyo, sio wimbo wa Nchi yangu mwingine.

Katika ushahidi wake, Ditto pia aliwasilisha 'Flash Disc' yenye 'audio' na 'video' za matangazo anayolalamikia na nyimbo hiyo ambayo alidai yeye ndiye mmiliki halali.

Kabla ya Mahakama hiyo kupokea kielelezo hicho, wakili wa Multi Choice Tanzania Limited, Mlekano alihoji uhalali wa video hizo kama si za kutengenezwa.

Kwenye ushahidi wake, Ditto alidai ni halali na endapo 'links' za matangazo hayo hazijafutwa, Mahakama iridhie waangalie kwenye mtandao, na Jaji Mwanga aliliridhia ombi hilo, na video hiyo ilipochezwa, ikafunguka na kumuonyesha mchezaji wa zamani wa Simba na Yanga, Akida Mapunda akihamasisha Afcon huku akiwa na matangazo ya DSTV na katika (background) ulisikika wimbo wa Nchi Yangu.

Ditto pia aliwasilisha vielelezo vingine ambavyo Mahakama ilivipokea kama ushahidi wake.

Nje ya Mahakama, wakili wa Ditto, Elizabeth Mlemeta alisema kesi hiyo imeanza kusikilizwa na upande wa mdai una mashahidi watano.

"Leo (juzi), shahidi mmoja ambaye ni Ditto ametoa ushahidi, upande wetu tuna mashahidi watano ambao kesho (jana) wataendelea kutoa ushahidi, tuko hatua nyingine za kisheria ambazo zinaendelea.

"Kama mlivyomsikia mteja wangu, ameomba fidia ya kiasi hicho cha fedha na maombi mengine kama ambavyo Mahakama itaona ni sahihi,".

Alisema Ditto anailalamikia Kampuni ya MultiChoice kutumia wimbo wake bila ridhaa yake katika kipindi cha kampeni ya Afcon 2019.



Msanii wa muziki wa kizazi kipya, Lameck Ditto (katikati) akiwa nje ya Mahakama Kuu kanda Dar es Salaam muda mfupi kabla ya kusikilizwa kesi aliyoifungua dhidi ya Malti Choice Tanzania. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Ushindi wamuibua kiongozi Geita Gold

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Geita Gold kupata ushindi wa kwanza wa bao 1-0 ikicheza dhidi ya JKT Tanzania nyumbani Uwanja wa Nyankumbu, Geita juzi, Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Leonard Bugomola amesema siri kubwa ya ushindi huo ni kukaa pamoja na kuelewana.

Aidha, Bugomola amekiri kulikuwa na matatizo kidogo ndani ya timu hiyo ambayo sasa yamepatiwa ufumbuzi na kutatuliwa.

"Matokeo ya ushindi tumeyapokea vizuri kwa sababu tulikuwa hatujapata ushindi tukicheza nyumbani tangu mwanzo wa ligi kwa hiyo tunamshukuru Mungu.

"Tatizo ni mawasiliano tu na kukaa kwa pamoja, mwanzo kulikuwa na shida kidogo naamini baada ya kuwa tumekaa kwa pamoja tutasonga mbele, tutakaa vizuri kama unavyoona,"alisema mwenyekiti huyo.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 42 likiwekwa wavuni na Edmund John lililoifanya timu hiyo kupata ushindi kwa mara ya kwanza ikicheza nyumbani baada ya mechi tisa.

Geita ilicheza idadi hizo za mechi ikitoa sare mechi mbili nyumbani na kupoteza michezo miwili huku ikishinda mchezo mmoja ugenini na kutoka sare michezo miwili.

Timu hiyo imefikisha pointi 10 katika michezo 10 ambayo imecheza ikiwa ni wastani wa pointi moja kwa kila mechi.

## Simba yajitetea kufungiwa kusajili

INATOKA UK. 24

wowote kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kuanza Desemba 16 hadi Januari 15 mwakani.

Kifungo hicho kimekuja wakati uongozi wa klabu hiyo ukijiandaa kufanya maboresho ya timu hiyo inayoshiriki Ligi ya mabingwa Afrika.

## Gamondi: Tupo tayari, hatuna presha

INATOKA UK. 24

dhidi ya USM Alger ya huko miezi mitano iliyopita kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Ilikuwa ni Juni 3 kwenye uwanja huo wa Juillet wa Tano iliposhinda bao 1-0 lililofungwa kwa mkwaju wa penalti na Djuma Shaaban dakika ya saba ya mchezo, ingawa haliku-weza kuwafanya kutwaa ubingwa huo, kwani katika mechi ya kwanza jijini Dar es Salaam, ilifungwa mabao 2-1, hivyo kukosa ubingwa kwa bao walilofungwa ugenini.

Leo Yanga itacheza hatua hiyo ya Makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya miaka 25 kwani mara ya mwisho kufanya hivyo ilikuwa mwaka 1998.

Katika hatua hiyo Yanga ilikuwa pamoja na timu za Raja Casablanca ya Morocco, Asec Mimosas ya Ivory Coast na Maning Rangers ya Afrika Kusini ambapo iliburuza mkia.



Michezo

Ijumaa Novemba 24, 2023

Nipashe



Ditto aidai fidia Multi Choice Tanzania UKURASA 23

# SIMBA SC YAJITETEA KUFUNGIWA KUSAJILI

●●●Yakiri haikuwa na mawasiliano na klabu ya zamani ya Sakho ambayo ime...




**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema kuwa ulipanga kuilipa klabu ya Teungueth ya Senegal kwenye awamu ya pili ya malipo wanayoyasubiri kutoka klabu ya Quevilly Rouen Metropole ya Ufaransa iliyomnunua mshambuliaji wao wa zamani Pape Osman Sakho.

Shirikisho la Soka Tanzania jana lilitoa taarifa kuwa Simba imefungiwa na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) kufanya usajili wa wachezaji wa kimataifa baada ya kushindwa kuilipa klabu hiyo ya Senegal malipo ya asilimia 15 ya mauzo ya Sakho kwenda Ufaransa.

Katika taarifa hiyo ya TFF iliyotolewa na Ofisa Habari wake, Cliford Ndimbo ilieleza kuwa baada ya FIFA kutoa adhabu hiyo, TFF nayo imeifungia Simba kufanya usajili wowote wa wachezaji wa ndani mpaka itakapoilipa timu hiyo.

"Klabu hiyo ilifungua kesi FIFA dhidi ya Simba ikidai sehemu ya malipo kutokana na mauzo ya Sakho na ilitakiwa iwe imetekeleza uamuzi huo ndani ya siku 45 lakini haikufanya hivyo.

"Wakati FIFA imeifungia klabu hiyo kufanya uhamisho wa wachezaji wa kimataifa, TFF imeifungia kufanya uhamisho wa ndani," ilisema sehemu ya taarifa hiyo ya TFF.

Muda mchache baada ya TFF kutoa taarifa hiyo, Uongozi wa Simba ulitoa maelezo huku ikikiri kutofanya mazungumzo na klabu hiyo ya Senegal hali iliyopelekea kushtakiwa FIFA.

Simba ilipaswa kuilipa Teungueth asilimia 15 ya mauzo ya Sakho kwenda kwenye klabu hiyo ya Ufaransa lakini haikufanya hivyo na kupelekea Wasenegal hao kuishtaki Simba FIFA.

Taarifa ya Simba iliyotolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Imani Kajula ilisema kuwa walikuwa wakisubiri kupokea malipo yao ya awamu ya pili kutoka Quevilly Rouen Metropole ili wawalipe Wasenegal hao.

"Tunakiri hatukuwa na mazungumzo na Teungueth na hali hii ilipelekea wenzetu kutushtaki, lakini Simba inafanyia kazi suala hili tutailipa klabu hiyo hivi karibuni," alisema Kajula kwenye taarifa hiyo.

Alisema makubaliano ya mauzo ya Sakho ilikuwa Simba kupokea malipo kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza walipokea asilimia 50 ya malipo hayo na walikuwa wakisubiri awamu ya pili ndipo watoe fedha kuwalipa Teungueth.

Sakho alijiunga na Simba 2021 akitokea timu hiyo ya Senegal na kuitumikia hadi mwaka huu, ambapo kabla ya msimu mpya kuanza aliuzwa kwenye klabu hiyo ya Ligi Daraja la Pili nchini Ufaransa.

Taarifa kutoka vyanzo vingine zinasema kuwa wakati klabu hiyo ya Senegal inamuuza katika klabu ya Simba kuliwekwa kipengele cha kulipwa sehemu ya pesa kama mchezaji huyo atauzwa kwa timu nyingine.

Kwa hatua hiyo kama Simba hawatalipa pesa hiyo haitafanya usajili

INAENDELEA UK. 23

# Gamondi: Tupo tayari, hatuna presha

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI leo usiku wakishuka kwenye uwanja wa Juillet wa tano nchini Algeria kucheza mchezo wao wa kwanza hatua ya Makundi Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi amesema kuwa wapo tayari kwa mchezo huo na hawana presha.

Gamondi, alisema kuwa amewasoma wapinzani wao na anajua ubora na udhaifu wao na sasa kazi imebaki kwa wachezaji wake kufanya kile alichowaelekeza.

"Sitaki kuwapa presha wachezaji wangu, tunajua tutawakabili vipi wapinzani wetu, tunataka kuanza vizuri kwenye hatua hii na kazi kwa sasa imebaki kwa wachezaji wangu kufanya kile nilichowaelekeza," alisema Gamondi.

Aidha, alisema licha ya kucheza ugenini hawana presha yoyote na mchezo huo utakaoanza saa 4:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

"Yanga ilicheza hapa (Algeria) miezi mitano iliyopita tena kwenye hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, wanauzoefu na mechi hizi, hatuna presha na tupo tayari kukabiliana nao," alisema Gamondi.

Alisema mashabiki wa timu hiyo waendelee kuiombea na kuitakia mema na wao kama timu hawatawaangusha na watalipa fadhila za kuwasapoti kwa kufanya vizuri kwenye mchezo huo.

Yanga itashuka kwenye uwanja ambao ina kumbukumbu nao nzuri iliposhinda bao 1-0

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >